# Nipashe

Jumatatu Juni 22, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580264

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

215779502

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN




## Wahadhiri waibua siri chanzo cha rushwa ya ngono vyuoni

UKURASA 16

### BAA LA CORONA



Wazee na watu wenye magonjwa ya kudumu kama shinikizo la damu, kisukari, matatizo ya figo ndiyo walio kwenye hatari zaidi ya kuathirika pindi wanapopatwa na virusi vya Corona. WHO.

- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

# Membe asubiria Kamati Kuu CCM

- Ataka kuweka wazi uamuzi wa kumfukuza, vinginevyo achukue fomu za urais wakati wowote...

*Uk. 2*




Mtangaza nia ya urais wa Zanzibar kupitia CHADEMA, Muhammed Ayoub Haji (kulia), akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho Kikwajuni Zanzibar kutangaza nia ya kugombea uraisi. **KUSHOTO:** Aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango wa Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, baada ya kuchukua fomu ya kuwania uteuzi wa CCM kugombea urais wa Zanzibar, jana. **PUCHA ZOTE: RAHMA SULEIMAN**

## MSAJILI ATIA NENO VYAMA KUSHIRIKIANA UCHAGUZI MKUU

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## CCM wafikia 15 urais Z'bar, watatu CHADEMA watia nia

UK. 2


MICHEZO YANGA, AZAM ZAIBEBA SIMBA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

**HABARI KITAIFA**

# Msajili atoa neno vyama kushirikiana

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Msajili wa Vyama vya Siasa, imesema vyama ambavyo vinataka kushirikiana kwenye uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba, mwaka huu vimeshachelewa kwa mujibu wa sheria.

Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, aliyasema hayo jana katika mahojiano maalum yaliyolenga kujua msimamo wa ofisi hiyo, kuhusu suala la ushirikiano wa vyama vya siasa wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Akijibu kuhusu suala hilo, Nyahoza alisema mpaka sasa ofisi yake haijapokea mkataba wa makubaliano ya ushirikiano kutoka kwa chama chochote cha siasa.

Hivyo, alisema kwa mujibu wa sheria vyama ambavyo vina nia ya kushirikiana vimeshachelewa.

"Ipo sheria iliyoainishwa kwenye Kifungu namba 11 (a) cha sheria hivyo kama vyama havitaifuata vitakuwa vimeivunja. Vyama vya siasa vinavyotaka kushirikiana bila kufuata sheria hii vitakuwa vimeivunja.

Alifafanua kuwa, ushirikiano wa vyama umeratibiwa vizuri kisheria ambapo vyama vinapohitaji kushirikiana vinapaswa kutumia vikao halali vya chama badala ya utashi wa mtu binafsi.

"Baada ya vikao halali kupitisha azimio la kufanya ushirikiano, vyama husika vinapaswa kuwasilisha mkataba wa ushirikiano katika ofisi ya msajili ofisi miezi mitatu kabla ya mchakato wa uchaguzi kuanza," alisema.

Alisema vyama havijakatazwa kushirikiana bali vimewekewa utaratibu ili Tume ya Uchaguzi pamoja na taasisi zote zinazohusika ziweze kujiandaa vizuri na kuimarisha ulinzi hasa wakati wa kampeni.

Pia, alisema lengo lingine ni kuvisaidia vyama vingine kuelewa wanashindana na chama gani.

Alisema hadi sasa vyama vyenye usajili wa kudumu ni 19 na kimoja kina usajili wa muda, na maombi ya vyama 16 bado yanafanyiwa upembuzi.

# Membe asubiria Kamati Kuu CCM

**Na Enock Charles**

KADA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambaye ni Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, ameitaka Kamati Kuu ya Chama CCM itamke kuwa kile alichoita kuwa ni mapendekezo yao ya kumfukuza uanachama kuwa yalitolewa kwa bahati mbaya.

Akizungumza na wananchi mkoani Lindi, Membe amedai kuwa uamuzi wa kumfukuza yeye yalikuwa ni mapendekezo ambayo yalipaswa kupelekwa Halmashauri Kuu (NEC), hivyo ameitaka kurejelea uamuzi wao kwa vile mapendekezo yao yalienda kwa jamii kwa bahati mbaya.

"Kwa kuwa Kamati Kuu tunaiheshimu ,tunamheshimu Mwenyekiti na tunaiheshimu Kamati Kuu , itamke iseme kwamba kile tulichokisema sisi wakati ule ni mapendekezo ni bahati mbaya yalitoka nje ni mapendekezo ambayo yatafanyiwa kazi na halmashauri Kuu ya Taifa mwezi ujao," Membe alisema

"Wakitamka hivyo leo ama wakitamka hivyo kesho, tutajaza kugombea urais Jumatatu asubuhi."

Chama hicho tawala kilimfukuza Membe uanachama kwa kile alichodai ni utovu wa maadili baada ya kuvuja kwa sauti ya kada huyo pamoja na makada wengine ikiwamo waliowahi kuwa Makatibu Wakuu katika chama hicho Abdulrahman Kinana na Yusuph Makamba katika mitandao ya kijamii wakizungumzia mienendo ya chama hicho katika uongozi wa awamu ya tano.

Hata hivyo, baadhi ya makada akiwamo January, Makamba, Nape Nnauye, Yisif Makamba na William Ngeleja walisamehewa.

Kinana aliomba radhi, lakini hajasamehewa wakati Membe alifukuzwa uanachama, lakini amekataa kuomba radhi akisema haoni kosa alilolifanya.

Wengine walisamehewa baada ya kuomba msamaha na kukiri makosa yao huku wengine wakiwekwa chini ya uangalizi wa mwaka mmoja na kupewa onyo kali na chama hicho tawala.

Akizungumza na wananchi hao wa Lindi, Membe alidai kuwa mchakato wa uchaguzi ndani ya Chama hicho tawala hauwezi kunoga bila yeye kugombea huku akiwadokeza wananchi hao kuwa kabla ya kufikia Oktoba mwaka huu ambapo uchaguzi utafanyika, chochote kinaweza kutokea.

Membe pia aligusia suala la tume huru ya uchaguzi akisema kuwa uchaguzi hauwezi kuwa huru na wa haki kama tume ya uchaguzi haitafanyiwa marekebisho, akirejelea madai ya muda mrefu ya vyama vya upinzani na baadhi ya makundi katika jamii kuwa wengi wa watendaji wa tume ni makada wa chama tawala .

"Kuna wakati nikafikiri uchaguzi huu hautafanyika karibuni, lakini wanasiasa wengine wakasema hapana, tukazanie moja tu la kuwa na tume huru ya uchaguzi na kuwa na waangalizi wa uchaguzi mambo mawili lakini tuendelee kuwa na uchaguzi."

Uchaguzi Mkuu unatarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu na tayari vyama mbalimbali vimeshaanza michakato ya ndani ya vyama vyao kualika wagombea kwa nafasi za urais, ubunge, udiwani .

Membe amewahi kushika nyadhifa mbalimbali katika Serikali ikiwamo nafasi ya uwaziri katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika Serikali ya awamu ya nne chini ya Rais Jakaya Kikwete akiwa ni wa pili kukaa katika Wizara hiyo kwa muda mrefu zaidi baada ya Rais Jakaya Kikwete ambaye alikaa miaka 10 mfululizo, Membe alikaa katika Wizara hiyo kwa miaka nane.

Membe pia alikuwa mbunge wa jimbo la Mtama na aliachia nafasi hiyo mwaka 2015 alipoamua kugombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo hata hivyo, aliishia nafasi ya tano bora mwaka 2015.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, (kushoto) akiangalia picha kwenye mashine ya BVR pamoja na Mwanamisi Mbuva, mkazi wa kitongoji cha Mtungumu jijini Dodoma, alipokuwa akiboresha taarifa zake katika daftari la kudumu la wapigakira. Wa tatu kulia ni Mwandikishaji "BVR Operator" Bi. Leila Nyundo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Warithi wa Shein wafikia 15 CCM, 3 watia nia CHADEMA

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDADI ya makada wa CCM wanaotaka kumrithi Rais wa Zanzibar, Dk Ali Mohamed Shein, inazidi kuongezeka baada ya jana aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango wa Zanzibar, Dk.Khalid Salum Mohamed, kuchukua fomu na kufikisha idadi ya wagombea 15.

DK. Khalid ambaye ni Mwakilishi wa jimbo la Donge, mkoa wa Kaskazini Unguja, alichukua fomu na kukabidhiwa na Katibu Kamati Maalumu Idara ya Oganizesheni, Galous Nyimbo, jana saa 8:00 mchana katika ofisi kuu za CCM Kisiwandui.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukabidhiwa fomu hiyo, alisema kuwa ameamua kufanya uamuzi huo kwa sababu ana uwezo wa kuitumikia CCM na wananchi wa Zanzibar.

Alisema pia ana nguvu za kufanya kazi hiyo mambo hayo yamemsukuma kuchukua fomu iwapo atapata ridhaa atawatendea haki wananchi.

"Najitokeza kuingia katika mchakato huu, naomba kutumwa na wananchi na ninao uwezo huo wa kutatumikia,"alisema.

Alieleza kuwa atahakikisha Mapinduzi ya Zanzibar yanaendelezwa na atadumisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ni muhimu kwa maendeleo.

"Tunashiriki katika kinyang'anyiro hiki kwa sababu tuna demokrasia ndani ya chama chetu ... nampongeza rais wa Zanzibar na Tanzania kwa utekelezaji mzuri wa ilani ya CCM," alisema.

Mwaka 2006, aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Dk.Amani Abeid Karume, alimteua kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Kazi, hadi mwaka 2008 alihamishiwa katika Wizara ya Kilimo na kuwa katibu mkuu na ilipofika mwaka 2010 alipelekwa katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na kuwa kiungo kikuu katika masuala ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano.

Akiwa katika Ofisi ya Makamo wa pili wa rais alifanya kazi kubwa katika kushughulikia utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa ajili ya kuratibu masuala ya kaya masikini ambayo Zanzibar imefanya vizuri sana.

Hadi jana wagombea 15 walikuwa wameshachukua fomu akiwamo,Mbwana Bakari, Balozi Ali Karume, Mbwana Mwinyi Yahya, Omar Shehe,Muhammed Jafar na Muhammed Hija.

Wengine ni Meja Jenerali, Issa Suleiman Nassor, Shamsi Vuai Nahodha, Dk Hussein Mwinyi, Prof. Makame Mbarawa, Mwatum Mussa Sultan, Haji Rashid Pandu, Dk. Abdul-halim Mohammed Ali, Jecha Salim Jecha na Dk. Khalid Salum Mohamed.

**WATATU WATIA NIA CHADEMA**

Wakati huo huo, Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetangaza majina matatu ya makada wa chama hicho waliotia nia ya kugombea urais wa Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkurugenzi wa Oganaizesheni wa Chama hicho Zanzibar, Kado Salim, aliwataja Makada hao ni Hashim Juma Issa ambae ni Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Taifa wa chama hicho, Mohd Ayoub Haji ambaye ni Mwenyekiti wa Mkoa wa Kusini Unguja pamoja na Said Issa Mohd makamu Mwenyekiti wa Chama Zanzibar .

## HABARI KITAIFA

# Majaliwa aipa maagizo mazito TAKUKURU uchaguzi Oktoba

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Serikali imewaagiza makamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wahakikishe wanawakamata na kuwachukulia hatua watu wote watakaojihusisha na vitendo vya rushwa kuelekea uchaguzi mkuu.

"Watu wamezoea vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi, Serikali tumeagiza kwa kamati za ulinzi na usalama zishirikiane kuhakikisha kwamba hakuna vitendo vya rushwa katika uchaguzi na yeyote ambaye anajihusisha na rushwa asiachwe."

Alitoa kauli hiyo juzi jioni wakati akizungumza na viongozi wa mkoa wa Lindi baada ya kuwasili katika uwanja wa ndege wa Nachingwea akiwa njiani kuelekea wilayani Ruangwa kwa ziara ya kikazi.

Waziri Mkuu alisema kitendo cha kutoa na kupokea rushwa ni kosa, hivyo viongozi hao wa TAKUKURU nchini hawanabudi kuwachukulia hatua watu wote watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo.

Vilevile, Waziri Mkuu aliwataka Makamanda wa TAKUKURU katika wilaya zote nchini wahakikishe wanawakamata watu wote watakaojihusisha na vitendo vya rushwa wakiwamo wapambe ambao ndio wachochezi wa vitendo hivyo.

Alitoa maagizo hayo ili kuhakikisha uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu unakuwa huru na wa haki, hivyo kuwawezesha wananchi kuchagua viongozi wanaowahitaji na si kwa msukumo wa rushwa.

Katika hotuba yake ya Juni 15, 2020 bungeni jijini Dodoma wakati akihitimisha mkutano wa 19 wa Bunge, Waziri Mkuu aliwataka viongozi wa vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi wazingatie katiba, sheria, kanuni na miongozo iliyopo katika uendeshaji wa shughuli za uchaguzi.

Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo kuwasihi viongozi na wanachama wa vyama vyote vya siasa na wananchi kwa ujumla waendelee kulinda amani na kuendeleza mshikamano katika kipindi hiki na wakati wa uchaguzi mkuu.



Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika mkoa wa Mtwara, (MAMCU) Joseph Kitando (wanne kushoto), akisoma taarifa ya ugawaji wa pembejeo za kilimo na mkopo kwa wakulima (hawapo pichani), ambapo wakulima hao wamekopeshwa sulpha ya unga jana, wilayani Masasi kwa ajili ya maandalizi ya msimu huu. Wengine ni viongozi wa Chama Kikuu Cha Ushirika wa Wakulima Masasi-Mtwara (MAMCU), akiwamo Meneja wa Chama hicho tawi la Masasi, Joseph Mmole (wa kwanza kushoto).. **PICHA: HAMISI NASRI**.

# Wakulima wa korosho wakopeshwa pembejeo

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

WAKULIMA wa Korosho wa Chama cha Ushirika cha MAMCU, wamekopeshwa pembejeo za kilimo zaidi ya tani 1,500 za salfa ya unga.

Lengo la kukopeshwa ni kuhakikisha kuwa wanaongeza tija ya uzalishaji wa korosho kwa msimu wa 2020/2021.

Wakulima hao walipatiwa mkopo huo jana wilayani Masasi, baada ya chama hicho kuzindua rasmi mchakato wa ugawaji wa pembejeo za kilimo kwa mkopo kwa wakulima wake kupitia vyama vyao vya ushirika vya msingi.

Akisoma taarifa ya ugawaji wa pembejeo hizo, Meneja wa MAMCU tawi la Masasi, Joseph Mmole, alisema katika kuelekea msimu mpya wa zao hilo la korosho, MAMCU kimeamua kuwapatia mkopo wa pembejeo za kilimo wakulima wake ambayo ni salfa ya unga kwa bei ya Sh.32,000 kwa mfuko mmoja.

Alisema hadi sasa tayari wameshasambaza kilogramu 699,000 ambayo ni sawa na mifuko ya Salfa 27,960 kwenye vyama vya msingi vya ushiria 72 ambavyo ni wanachama wao.

Alisema moja ya faida ya mkopo huo kwa wakulima ni kwamba mkulima atafanya marejesho ya fedha baada ya mauzo ya korosho zake katika msimu huo.

"Matarajio yetu hadi kufikia mwishoni mwa mwezi huu tutakuwa tayari tumeshamaliza kusambaza pembejeo zote kwa wakulima kupitia kwenye vyama vyao vya ushirika,"alisema Mmole.

# Magufuli awataka CCM kufanya mageuzi jimbo la Mch. Msigwa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amewataka wanachama wa chama hicho mkoani Iringa, kuhakikisha wanafanya mageuzi kwa Jimbo hilo katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika oktoba mwaka huu.

Magufuli alitoa agizo hilo wakati akizungumza kwa njia ya simu na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Humphrey Polepole, aliyekuwa akifanya mkutano na wanafunzi wa vyuo vikuu mkoani humo.

Jimbo la Iringa mjini linaongozwa na Mbunge wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mchungaji Peter Msigwa.

Magufuli akizungumza na wanafunzi hao kwa njia ya simu alisema: "Nasema CCM hoyee kwa kuwa mpo Iringa nasema kamwene, basi nawashukuru sana vijana, endeleeni kuchapa kazi, ni mwaka wenu na Mungu awajalie sana endeleeni kukitetea Chama Cha Mapinduzi, ninawapenda vijana na Mungu awasaidie sana katika kuchapa kazi na ninyi ndio mnaleta jeuli ya Chama Cha Mapinduzi."

Magufuli alisema anafurahi Umoja wa Vijana wa CCM Iringa wanavyofanya kazi nzuri, hivyo ni matumaini yake wataendelea kufanya kazi na hata kuhakikisha jimbo hilo la Iringa mjini linarejea mikononi mwa CCM kwenye uchaguzi mkuu.

"Mpo kwenye Jimbo la Iringa kwa wapinzani na nitafurahi kuona vijana wa UVCCM Iringa wanafanya kazi nzuri, nimepata taarifa zao asanteni sana," alisema Rais Magufuli.

Akizungumza na vijana, Polepole alisema kuwa muda wa mbunge Msigwa kuendelea kwenda bungeni umekwisha, sasa ajiandae kwenda kusimamia mashamba yake ya nyanya na kanisa lake kwani ubunge wa jimbo hilo ameshapoteza.


**CHETI CHA USAJILI KIMEPOTEA**

**TAASISI YA KIISLAM MKOA DODOMA** anatangaza kupotelewa na CHETI CHA USAJILI **NO. 2438 YA 26/11/1958** kilichotolewa kwa jina la **THE DODOMA GENERAL MUSLIM ASSOCIATION** tarehe 05/05/2016 huko kata ya VIWANDANI DODOMA.Yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/RB/13663/2016.**

215783202



**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 35 OF 2020**

**In the Matter of the Estate of the late MARTHA DAUDI ELISHA of BUIGIRI Area within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SHELA KENETH DENDE**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 23 Day of JUNE, 2020.

Date at Dodoma this 12th Day of May, 2020

RESIDENT MAGISTRATE

115783102



**Enabel** Belgian Development Agency

**PRE-BID MEETING FOR UPCOMING CONSTRUCTION TENDERS**

Enabel, the Belgian Development Agency, through Water Sanitation and Kigoma Region Project (WASKIRP) plans to engage contractors and consultants for construction of water supply networks in Kigoma region. Several tenders are currently being prepared for publishing. Enabel therefore has organized a meeting for interested contractors and consultants for orientation to the bidding documents and processes so as to achieve appropriate responsiveness to the tenders. The meeting will be held as follows:

**Date** : **Saturday, 27 June 2020**

**Venue** : **Hotel Slipway, Slipway Road, Msasani Peninsula, Dar es Salaam**

**Time** : **10:00 – 14:30 PM**

The meeting will allow a maximum of 2 people per company. Interested companies are encouraged to submit their interest and names of their representatives by Thursday, 25th June 2020. No company will be allowed to be represented in the meeting if they fail to register their interest to attend the meeting and if they do not submit their names before this date.

In the wake of the COVID 19 situation, the meeting will adhere to strict preventative measures as guided by the government for such meetings. All participants are required to bring facial masks to wear while the organizers will ensure availability of sanitization fluids and hand washing facilities.

Submit your interest to participate in the meeting and the name(s) of your company representative through email to **constantin.hien@enabel.be** copying to **lilian.ayo@enabel.be**

215780102

# TPSF yaipa serikali vifaa tiba vya bil. 2/-

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa sekta binafsi nchini wamekabidhi vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni mbili kwa wizara ya afya, Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto kwa ajili ya vituo mbalimbali hapa nchini.

Wametoa vifaa hivyo kama sehemu ya kutambua na kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha sekta ya afya na kukabiliana na maambukizi ya corona.

Akizungumza baada ya kukabidhi vifaa hivyo

kwa Mganga Mkuu wa Serikali , Prof Abel Makubi,

Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta ya Binafsi Tanzania (TPSF), Angelina Ngalula, alisema sekta binafsi kama mdau wa maendeleo, imeguswa na juhudi hizo.

"Sisi sekta binafsi tunatambua na tunaunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano, na ndiyo maana tupo mstari wa mbele kuchangia vifaa tiba ambavyo vitakwenda kutumika

katika kutoa huduma bora za matatibu kwa jamii," alisema Ngalula.

Aliwataka wadau na wafanyabiashara kuendelea kuiunga mkono

serikali kwa kuchangia maendeleo ya sekta binafsi kwani hatua kubwa imefanywa katika kujenga miundombinu kwenye sekta ya afya, hivyo ni jukumu lao kurudisha kile tunachokipata kwenye shughuli zao kwa jamii.

"Vifaa ambavyo vimetolewa na wadau wa sekta binafsi nchini ni pamoja na magodoro, vitanda, vifaa vya kufanyia upasuaji, sabuni na pesa taslimu ambazo zitatumika kutoa huduma kwenye vituo mbalimbali vya afya vilivyojengwa hapa nchini," alisema Ngalula.

Akipokea vifaa hivyo kwa niaba ya Waziri wa wizara hiyo, Ummy Mwalimu, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Makubi aliwashukuru wadau wa sekta binafsi nchini kwa kuona umuhimu wao kwa kuchangia vifaa tiba pamoja na fedha kwa Wizara ya Afya.

Prof Makubi alisema Serikali imepiga hatua kwa kuboresha upatikanaji wa huduma ya afya na ndiyo maana vimejengwa vituo vya afya vingi katika awamu hii ya tano ukilinganisha na awamu zilizopita huku lengo kuu ni kuiboresha sekta ya afya.

# Sababu wabunge 21 CUF kujiunga na ACT

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Malindi visiwani Zanzibar, Ally Saleh, ameeleza sababu zilizowasukuma yeye na wabunge wenzake 20 na madiwani tisa wa Chama cha Wananchi (CUF), kujiunga na chama cha ACT-Wazalendo.

Juzi, wabunge hao walipokewa jijini Dar es Salaam na viongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, akiwamo Maalim Seif Sharrif Hamad, Mwenyekiti wake na Zitto Kabwe, Kiongozi Mkuu wa chama hicho.

Akizungumza kwa niaba ya wabunge hao, Saleh alisema wamejiunga na chama hicho baada ya kuona CUF imepoteza nguvu ya kuhimiri vishindo vya siasa.

Saleh alisema wanaanza upya ndani ya ACT-Wazalendo, huku akijigamba kwamba wamejipanga kutetea majimbo yao kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Vilevile, Saleh alisema walitamani kujiunga na ACT-Wazalendo pamoja na Maalim Seif na wafuasi wake kupitia kampeni ya 'Shusha Tanga, Pandisha Tanga', lakini walishindwa kutokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wao.

Wimbi la wanachama wa CUF kutimkia ACT-Wazalendo lilishika kasi tangu Machi, mwaka jana baada ya kuibuka kwa mgogoro wa kiuongozi baina ya Maalim Seif, aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, na Profesa Ibrahim Lipumba, Mwenyekiti wa CUF.

Mbali na Saleh, wabunge wengine wa CUF waliotimkia ACT-Wazalendo na majimbo yao kwenye mabano ni pamoja na: Suleiman Bungara, maarufu Bwege (Kilwa Kusini); Juma Kombo Hamad (Wingwi); Masouda Abdallah Salim (Mtambile); Ally Salim Khamis (Mwanakwerekwe); Hamad Salim Maalim (Kojani); Khalifa Mohamed Issa (Mtambwe); Mohamed Juma Khatibu (Chonga); Twahir Awesu Mohamed (Mkoani); Khatib Said Haji (Konde).

Wengine ni: Haji Khatib Kai (Micheweni); Othaman Omar Haji (Gando); Dk. Suleiman Ali Yussuf (Mgogoni); Mbarouk Salim Ali (Wete), Nassor Suleiman Omar (Ziwani); Yussuh Salim Hussein (Chambani); Abdallah Haji Ali (Kiwani); Yussuf Haji Khamis (Nungwi); Mohamed Amour Mohamed (Bumbwini); na Mgeni Jadi Kadika (Viti Maalum).




Mkurugenzi wa Shirika la Uzikwasa, Novatus Urassa (kushoto), akikabidhi vifaa tiba na kinga kwa uongozi wa wilaya ya Pangani juzi vyenye thamani ya Milioni 42. Katikati ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Pangani, Mwalimu Hassani Nyange, ambapo vifaa hivyo vilivyotolewa kwa shirika hilo kupitia wafadhili wao Irish Aid. **PICHA: OSCAR KASMIRI**.

# Benki za NIC na CBA zaungana

**Na Mary Geofrey**

BENKI ya NIC Tanzania Limited (NIC) na benki ya Commercial of Africa (CBA) zimeungana na kuwa Benki ya NCBA Tanzania kwa ajili ya kuanza kutoa huduma kuanzia Julai 8, mwaka 2020.

Utekelezezaji wa kuungana utakuwa kwa kuhamishwa kwa mali na dhima, ambazo zimekwisha idhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT)na Tume ya Ushindani na baada ya kukamilika kwa mchakato wa kuungana taasisi mpya, benki ya NCBA itachukua dhamana zote, majukumu na haki zote za umiliki wa mali zilizohamishwa kutoka benki ya CBA kwenda benki mpya ya NCBA.

Kadhalika, itapokea wateja na madeni yote yaliyopo katika benki ya CBA na ziko katika mchakato wa kuhitimisha masharti mengine kutoka kwa mdhibiti.

Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya CBA, Gift Shoko, akizungumza jana kuhusu kukamilika kwa taratibu za kuungana kwao, alisema BOT imezipatia kibali cha kuungana mapema mwaka huu.

Alisema kibali kilitolewa katika barua iliyosainiwa Februari 14, mwaka huu na Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Dk. Bernard Kibesse.

Alieleza kuwa, baada ya mchakato kukamilika benki ya NCBA itakuwa benki ya daraja la na sehemu ya kundi la kampuni la NCBA Group PLC ambalo liliundwa Oktoba Mosi mwaka jana baada ya kupata kibali kutoka kwa Benki ya Kuu ya Kenya na Hazina ya Taifa ya Kenya kuidhinisha uunganaji wa kampuni hizo.

"Jina la benki ya NCBA linaashiria kuungana kwa benki mbili kubwa, benki ya NIC na CBA. Huu ni mwanzo wa safari mpya inayounganisha ubora wa benki zote mbili na kuunda taasisi kubwa na yenye nguvu zaidi ya kifedha na kuimarisha uchumi wa Tanzania," alisema Shoko.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa benki ya NIC, Margaret Karume, alisema mwezi ujao watakamilisha safari ya kuungana kwao na mchakato wa kuoanisha mifumo yao ili wateja waweze kufurahia huduma zisizo na usumbufu katika mtandao wa matawi yote nchini.

"Mkakati wetu wa uzinduzi vile vile utajumuisha ubainishaji wa utambulisho wa kundi jipya la mabenki la NCBA Group," alisisitiza Karume.

Kama sehemu ya ushirikiano wa kikanda wa NCBA Group, uunganishaji wa biashara nchini Rwanda ulikamilika mwanzo mwa mwaka huu. Pia kufika mwishoni mwa robo hii ya mwaka inatarajiwa pia kukamilika nchini Uganda.

## HABARI KITAIFA

# Chadema chasisitiza kutosusia uchaguzi mkuu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimesisitiza kuwa katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika oktoba 25, mwaka huu kitashiriki kwa asilimia mia katika nafasi zote, licha ya kuwapo kwa mazingira ya kufanyiwa figisu.

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho kutoka Bara, Benson Kigaila, aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa watiania wa nafasi ya ubunge kutoka Kanda ya Serengeti, inayounda mikoa ya Simiyu, Mara, pamoja na Shinyanga.

Alisema chama hicho katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka jana, kilijitoa kushiriki kwenye uchaguzi huo baada ya kuona kuwapo na mazingira ya kufanyiwa rafu na kwamba kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu mazingira ni hayohayo, na kusisitiza kuwa hakitajitoa bali kitapambana.

"Niwaambie tu watia nia wa nafasi ya ubunge na udiwani wa chadema, uchaguzi mkuu wa mwaka huu hakuna wa kujitoa, tuna jua kuna mazingira yameandaliwa ya kufanyiwa rafu, ambapo hakuna tume huru, katiba, na utungwaji wa sheria za kutubana, lakini tutapambana hivyo hivyo na tutashindia kituoni watake wasitake." alisema Kigaila na kuongeza:

"Tunachotakiwa ndugu zangu ni kwenda kupitisha wagombea ambao wanakubalika na wananchi na wenye moyo wa kuwatumikia katika kutatua matatizo yao, na watakaojenga hoja majukwaani, sababu tunajua wenzetu hawana hoja zaidi ya kujipanga kutumia dola na tukifanya hivyo tunawashinda kweupe," alisema Kigaila.

Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Serengeti, Ester Matiko, ambaye alikuwa mbunge wa Taarime mjini, nae ametia nia kutetea jimbo hilo, aliwatoa hofu watiania wenzake kwa kuwaeleza kuwa hakuna mgombea ambaye atashinda na asitangazwe.

Matiko aliwataka watiania wote kuungana na kuwa kitu kimoja na kumkubali yule ambaye atashinda kwenye kura za maoni ndani ya chama, na kupitishwa kuwa mgombea wa Jimbo au Kata na siyo kuunda makundi.

## Akatwa mkono kwa madai ya kuiba mahindi shambani

**Na Gideon Mwakanosyam** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linamshikilia mkazi wa kijiji cha Matimila, wilayani Songea, Faustine Haule (45), kwa tuhuma za kumkata mkono, Mariboti Nyoni (50) kwa kosa la kumuibia mahindi.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Ruvuma, Amin Mahamba, alisema inadaiwa siku hiyo ya tukio Nyoni alijeruhiwa kwa kukatwa mkono wake wa kulia na Mundu baada ya kukutwa akiiba mahindi shambani.

Alisema Juni 16, mwaka huu Haule alianza kuvuna mahindi shambani kwake na alilazimika kuyalinda kwa kulala shambani akiwa na mke wake kabla hajayasafirisha kupeleka nyumbani kwake Matimila.

Alisema Juni 20, mwaka huu majira ya saa 6 usiku, Haule akiwa analinda mahindi yake shambani akiwa na mke wake, ndipo ghafla walimuona Nyoni kwa kutumia mwanga wa tochi akiweka mahindi kwenye mfuko wa kiroba, ndipo alipokwenda kumkamata.

Alisema kuwa Haule alipofika jirani na Nyoni kutaka kumkamata, Nyoni alikaidi ndipo wakaanza kupigana.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushindani wahitajika zaidi katika soka nchini

**MCHEZO** wa soka ndio mchezo unaopendwa na wenye mashabiki wengi zaidi hapa nchini na ulimwengu.

Hapa nchini, Ligi Kuu Bara ndio ligi inayopendwa na kufuatiliwa na idadi kubwa ya mashabiki ambao wako ndani na nje ya Tanzania.

Ligi Kuu ndio ligi ya juu ambayo hutoa mwakilishi au wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambayo huchezwa kila mwaka chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Kwa sasa ligi hiyo inayoshirikisha timu 20 kutoka mikoa mbalimbali, sasa imeingia katika hatua ya lala salama.

Ili kupata mwakilishi bora wa Tanzania Bara katika mashindano hayo, ni lazima timu au klabu zitakazopata tiketi ya kupeperusha bendera ya nchi zipatikane kwa haki na kwa kupata pointi za uwanjani.

Endapo bingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara atapatikana kwa 'mizengewe' au 'kubebwa' kama ilivyozoeleka, basi safari ya mwakilishi huyo huenda ikaishia njiani mapema pale itakapokutana na wapinzani wao ambao wameimarika na walipatikana kwa haki.

Mbali na ligi hiyo, pia kuna mashindano ya Kombe la FA, michuano ambayo hutoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Lakini kabla ya kupata tiketi hiyo, timu huchuana katika mechi mbalimbali, kwa upande wa Ligi Kuu wakicheza nyumbani na ugenini, wakati Kombe la FA, lenyewe huchezwa kwa mfumo wa mtoano.

Hata hivyo, timu zinazoshiriki mashindano hayo zimekuwa zikishindwa kucheza katika kiwango kinachofanana na kusababisha baadhi ya michezo kutokuwa na ushindani na mvuto.

Timu, wachezaji au viongozi wa timu husika wamekuwa na tabia ya kuchagua baadhi ya mechi kwa kufanya maandalizi yasiyofanana na hali hiyo kutoa matokeo yasiyotarajiwa.

Nipashe inazikumbusha timu kufanya maandalizi yanayolingana na kufanana kwa kila mchezo, ili kusaidia kukuza viwango vya wachezaji wetu hapa nchini.

Kwa kufanya hivyo, itawasaidia wachezaji kucheza katika kiwango cha juu kwenye mechi zote, na kuacha 'kuitolea macho' baadhi ya michezo, huku huvuna pointi zinazofanana pale watakapoondoka na ushindi au sare.

Timu zinakumbusha kujipanga kusaka ushindi katika mechi zote, na kuacha 'kasumba' ya kupambana pale tu wanapojiandaa kuwakabili vigogo wa soka nchini, Simba au Yanga.

Ushauri huu si kwa timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, pia unazihusu timu zinazoshiriki Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Kuu Zanzibar, ambazo hutoa wachezaji wanaojiunga na Timu ya Taifa (Taifa Stars), kwa lengo la kupeperusha bendera ya nchi.

Endapo wachezaji watajipanga kuonyesha viwango vya juu katika mechi zote, tunaamini hata pale timu zao zitakapopata nafasi ya kutwaa ubingwa au kwenda kushiriki michuano yoyote ya kimataifa, Tanzania itakuwa imepata mwakilishi atakayekwenda kushindana na si kusindikiza wengine.

Umefika wakati wadau wa soka nchini wakabadilika na kujipanga kusaka ushindi katika kila mechi ambayo wanacheza na kuacha tabia ya kujiimarisha pale tu wanapokaribia kucheza dhidi ya Simba au Yanga.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Ni ngumu kudhibiti mashabiki viwanjani

**HIVI** majuzi serikali iliufungia Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma kuingiza mashabiki kutokana na kujaza idadi kubwa ya mashabiki, lakini pia kushindwa kufuata kanuni zilizowekwa na Wizara ya Afya juu ya udhibiti wa ugonjwa wa COVID-19 unaoletwa na virusi vya corona.

Hii ilikuwa ni baada ya mechi ya Jumatano iliyopita kati ya wenyeji JKT Tanzania dhidi ya Yanga iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1.

Kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara mashabiki walijazana kupita kiasi, baadhi wakiwa hawajavaa barakoa, lakini pia wakionekana wakikaa jirani na ile kanuni ya kuachiana mita moja haikuwapo.

Ingawa ugonjwa wa corona umepungua kwa kiasi kikubwa nchini Tanzania, lakini bado upo, na serikali inahitaji kuudhibiti ili kutoleta maambukizi mengi mapya kwa wakati mmoja.

Ilionekana kwenye picha za televisheni, JKT Tanzania ilipopata bao la kwanza jinsi mashabiki wao, ambao kiuhalisia ni wa Simba, walikuwa wakishangilia kwa staili ya kulala upande mmoja, halafu wa pili (kulia na kushoto). Hali hii ilisababisha mashabiki kugusana na kuegemeana.

Hali kadhalika, Yanga nayo iliposawazisha bao, mashabiki wao walipagawa kwa furaha na kushangilia kwa staili ambayo haikutofautiana na ya wenzao.

Kusema kweli hali ilivyokuwa ilikuwa ni hatari kwa afya za mashabiki wa soka katika mchezo huo.

Hata hivyo, kwa maoni yangu nadhani adhabu ya kuifungia JKT Tanzania kucheza mbele ya mashabiki wao ni kubwa na mbali na kuiathiri timu hiyo, pia mashabiki na wadau wa soka watakosa burudani na michezo mbalimbali ya Ligi Kuu.

Ukiangalia umati ule, karibu asilimia 90 ulikuwa ni wa mashabiki wa klabu mbili kubwa nchini, Simba na Yanga.

Sidhani hata kama Uwanja wa Jamhuri usingefungiwa, ungejaza tena mashabiki wengi kama siku ile, ikizingatiwa tayari imeshamalizana na Simba mechi zote mbili.

Mimi nilidhani wa kuadhibiwa wangekuwa na wasimamizi wa uwanja huo ambao walijaza watu kupita kiasi kilichowekwa.

Kuna taarifa kuwa baada ya kuingia watu kiasi kilichowekwa, mashabiki walianza kuingia kwa njia za panya, yaani kulikuwa na tiketi za magendo ambazo zilisababisha watu kuwa wengi kiasi kile.

Halafu ukiangalia, ni kwamba umati ule haukutofautiana sana na ule wa Juni 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kambarage mkoani, Shinyanga, wenyeji Mwadui walipocheza dhidi ya Yanga.

Mimi nadhani kama serikali imeruhusu mashabiki kuingia uwanjani, basi utaratibu uwe ni kwamba mashabiki wanaoingia wawe wamevaa barakoa, lakini pia kabla ya kuingia wanawe mikono na dawa, pia wasimamizi wawe makini kuwa na idadi maalum tu ya wanaingia na si vinginevyo.

Lakini tukisema watu wasikaribiane, kwenye mpira wa miguu ni ngumu sana.

Ikumbukwe soka ni mchezo wa hisia. Hata kama wakiruhusiwa watazamaji sita tu uwanjani, hutoona hata siku moja wamekaa mbalimbali. Ni lazima hao hao sita hata kama wamegawanyika, watatu wanashangilia timu moja na wengine nyingine, watakaa pamoja na kuanza kuzungumza, kutaniana, kujadili, kushangilia na makelele pia.

Umati wa mashabiki wa soka si umati waliokusanyika kwa ajili ya Injili.

Mashabiki wa soka siku zote wana mihemko, na wanataka wakae karibu karibu kwa ajili ya kuzodoana, wengine ambao ni timu moja watakaa ili kupeana moyo, kushangilia kwa pamoja na hata kusikitika kwa pamoja.

Hapa kuna mawili. Ni lazima tuamue ligi ichezwe bila mashabiki kama Ulaya, au kama tumeamua kama tulivyoamua, basi taratibu ziwe hizo nilizoziainisha na watu kunawa na kuvaa barakoa, lakini wakishaingia uwanjani na kukaa majukwaani, unaweza kuwadhibiti tu pale kabla mechi haijaanza, lakini ikianza wanakuwa si wale tena. Inakuwa ni ngumu sana kuwadhibiti wasikaribiane.



Mkuu wa Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, Philemon Sengati, (aliyevaa miwani), akipokea mbao na mabati ya kuezekea Kituo cha Afya cha Nsola kutoka kwa Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Donatus Richard (aliyevaa tai nyekundu). Vifaa hivyo vya thamani ya Sh. milioni 20 vimetolewa kukamilisha uezekaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# EFTA yawekeza kuinua sekta ya kilimo nchini

**Na Zuwena Shame**

TAASISI ya Usawa kwa Watanzania (Equity for Tanzania Limited-EFTA), imesema kuwa uwekezaji wa fedha na elimu kwenye sekta ya kilimo hasa kwa wakulima wadogo nchini kunaweza kuwa utatuzi wa changamoto ya sekta hiyo nchini.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa Masoko na Maendeleo ya Biashara wa EFTA, Peter Temu, alisema EFTA imetambua changamoto katika sekta ya kilimo nchini na hasa ukuaji wa uchumi na hivyo kuamua kuanzisha taasisi hiyo ili kusaidia wakulima wadogo wadogo.

Temu alisema kuwa kilimo kina mchango mkubwa kwa uchumi wa Tanzania na kuwa sekta hiyo imeonekana kuwa na changamoto kwa baadhi ya taasisi za mikopo na fedha.

Alisema kuwa EFTA Ltd ni mojawapo ya taasisi za kifedha zilizowekeza kiasi kikubwa sana kwenye kilimo na uchakataji mazao hapa nchini kwa kuelewa kuwa uchumi wa nchi yetu unategemea sana kilimo.

Alifafanua kuwa kilimo kwa Tanzania kinazalisha asilimia 90 ya chakula kinachohitajika ambapo asilimia 80 ya uzalishaji huo unatoka kwa wakulima wadogo wanaoishi vijijini na ambao teknolojia bado sio rafiki kwao au hawana kabisa zaidi ya kutegemea mvua na jembe la mkono.

"Hivyo tuliamua kuanzisha Taasisi hii kusaidia wakulima ikizingatiwa kuwa kilimo kinasaidia ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Tumewekeza zaidi ya Sh. bilioni 25 kwa kuwakopesha bila dhamana wakulima mashine mbalimbali za kilimo , matrekta na mashine zingine za kisasa ili kuondokana na changamoto ya kutumia jembe," alisema Temu.

Alisema pia EFTA imewekeza zaidi ya sh. bilioni tano katika kusaidia kuchakata mazao kwa wakulima wadogo na kuwafanya kubadili maisha yao kiuchumi.

Aliongeza kuwa kupitia EFTA wakulima wamebadili mfumo wao wa kilimo kwa kuzalisha kisasa zaidi na kwa wingi kwa kutumia matrekta na mashine zingine za kisasa zinazowafanya waondokane na kilimo cha zamani na kulima kisasa zaidi.

Temu alisema kuwa maisha ya wakulima wengi kupitia EFTA yamekuwa kiuchumi, mfano wameongeza mitaji, kusomesha watoto, kupanua biashara na kuongeza ajira kwa Watanzania, kuongeza uzalishaji na kuongeza thamani ya bidhaa za ndani na pia kuunga mkono dhamira ya serikali ya awamu ya tano ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda.

Hata hivyo ,Temu alisema EFTA imekuwa suluhu kwa wakulima wengi kwa sababu haitozi dhamana ya kitu ikilinganishwa na taasisi zingine za mikopo na fedha ambazo changamoto kwa baadhi ya taasisi hizo ni kutoza ongezeko la thamani (VAT) wakati wa huduma na ukodishaji wa vifaa.

Aliongeza kuwa kwa sasa EFTA umeanza kutoa mikopo katika sekta ya usafirishaji ikihusisha mabasi makubwa ya mikoani, daladala, malori makubwa na magari aina zote ya kufanyia kazi, pia sekta ya utalii tunakopesha magari ya aina mbalimbali kwa ajili ya kuwasafirisha na kuwahudumia watalii kama njia ya kuinua uchumi wa nchi kupitia utalii.

"EFTA tumepita hatua zaidi kwani kwa sasa tumesaidia kwenye sekta ya ujenzi na pia walengwa wanaweza kupata magreda, makatapila na vifaa vya aina yoyote vinavyotumika katika ujezi wa aina yoyote ile. Pia tuna mashine mbalimbali na magari yaliyotumika tunayoyakopesha kwa bei nafuu ili tu kusaidia Watanzania", alisema Temu.

EFTA Ltd ni kampuni ilianzishwa mwaka 2004 kwa lengo la kuwasaidia wajasiriamali na wakulima ambao walionekana kutokuweza kukopesheka na benki pamoja na taasisi zingine za kifedha.


HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

TANGAZO LA ZABUNI 2020/2021
ZABUNI Na. LGA/162/2020/2021/NC/01-07
KWA AJILI YA ZABUNI YA UWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO
Tarehe: 22/06/2020

1. Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu inawatangazia wananchi wote,Taasisi, Mashirika na watu binafsi kuwa inatarajia kukasimisha ukusanyaji ushuru wa mazao katika vyanzo vya geti la Kisuke, geti la Igunda, geti la Busenda, geti la Mpunze, geti la Mwabomba, geti la Imambona ushuru wa stendi ya mabasi Nyamilangano kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa kipindi cha kuanzia Agosti 2020 hadi Juni 2021.
2. Unakaribishwa kuleta maombi yako ukitaja kiasi cha fedha ambacho unaweza kukusanya na kuwasilishakwa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kwa kila chanzo unachoomba.
3. Vyanzo vya mapato vinavyotazamiwa kukasimishwa ni kama vinavyoonekana hapa chini:

A. ZABUNI ZA UWAKALA WA KUKUSANYA USHURU WA MAZAOKATIKA MAGETI, IKIWA NI MAZAO MCHANGANYIKO, MATUNDA NA STENDI YA MABASI.

| S/N | JINA LA ZABUNI | KIJIJI | KATA | NAMBA YA ZABUNI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ushuru katika geti la Kisuke | Kisuke | Kisuke | LGA/162/2020/2021/NC/01 |
| 2 | Ushuru katika geti la Igunda | Igunda | Igunda | LGA/162/2020/2021/NC/02 |
| 3 | Ushuru katika geti la Busenda | Busenda | Chona | LGA/162/2020/2021/NC/03 |
| 4 | Ushuru katika geti la Mpunze | Ifunde | Mpunze | LGA/162/2020/2021/NC/04 |
| 5 | Ushuru katika geti la Mwabomba | Mwabomba | Idahina | LGA/162/2020/2021/NC/05 |
| 6 | Ushuru katika geti la Imambo | Igalula | Ukune | LGA/162/2020/2021/NC/06 |
| 7 | Ushuru katika stendi ya mabasi Nyamilangano | Ididi | Nyamilangano | LGA/162/2020/2021/NC/07 |

4. Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-

I. Nyaraka za zabuni zinapatikana kwa kulipa ada ya Tsh 50,000/= ambazo hazitarejeshwa na zinapaswa kulipwa kwenye ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri yaWilaya ya Ushetu kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa tisa na nusu (saa 2:00 hadi 9:30 )alasiri kwa siku za kazi kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa. Kila uwakala utakaoomba unajitegemea, kwa uombaji wa uwakala wa kukusanya ushuru, wanashauriwa kutembelea eneo la Biashara kabla ya kuchukua nyaraka ya zabuni ambayo itatolewa katika ofisi ya katibu wa Bodi ya zabuni iliyopo katika jengo la ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, iliyopo kataya Nyamilangano.

II. Ombi la zabuni liwe na jina na anuani halisi ya mwombaji.Aidha aonyeshe mahali ofisi zake zilipo au anapoweza kupatikana (Physical Address).

III. Mwombaji aambatishekivuli cha leseni yoyote hai ya biashara ,TIN ya TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania).

IV. Mwombaji anatakiwa kulipia dhamana ya miezi miwili ya fedha taslimu ambayo ni sawa na kiasi atakachotaja kuwasilisha kwa kila mwezi.

V. Mwombaji atakayechaguliwa atalipwa asilimia kumi(10%) ya fedha atakazowasilisha kwa mwezi kulingana na kiasi kilichokubaliwa kwenye mkataba

VI. Zingatia kuwa fomu ya maombi ya zabuni inajazwa na kusaniniwa na mwenye uhalali wa kisheria (Power of attorney) katika zabuni hii.

VII. Mwombaji wa zabuni, endapo atachaguliwa atalazimika kulipa fedha za makusanyo yote kwenye akaunti ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu namba 30610004660, **UDC OWNSOURCE COLLECTION ACCOUNT** katika benki ya NMB- Kahama.

VIII. Makusanyo yote yatakusanywa kwa kutumia mashine za kielectronic (POS).

IX. Mwombaji awasilishe zabuni zote ziwe na nakala halisi moja (orginal) na nakala kivuli mbili zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa **NAMBA NA JINA LA ZABUNIHUSIKA**, kazi inayoombwa na anwani iliyotajwa hapo chini bila kuwekwa alama yoyote na kufungwa kwa lakiri.

X. Mwombaji atakayeshindwa masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima wa zabuni.

XI. Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu hailazimiki kuchagua zabuni yoyote.

XII. Zabuni zitawasilishwa kwa katibu wa bodi ya zabuni Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kwa anuani ifuatayo:

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**
**S.L.P 50, USHETU**
**KAHAMA**

XIII. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi haya ni tarehe 06/07/2020 saa 5.30 asubuhi siku ya Jumatatu. Maombi yote yatafunguliwa katikaofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya iliyopo kata ya Nyamilangano barabara ya Ulowa mbele ya wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuria katika ufunguzikwagharama zao wenyewe.

XIV.Zabuni zitakazochelewa ,zabuni zitakazo letwa bila viambatanisho, zabuni za kieletroniki, na kwa hali yoyote ile zabuni hizo hazitakubaliwa kwa ufunguzi. Aidha zabuni ikiishapokelewa haitakubalika kwa kwa marekebisho yoyote hali yoyote yale.

WANDERE P LWAKATARE
**Kaimu: MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**USHETU**

# Vijana ACT washangazwa Jecha kuwania urais CCM

Na Enock Charles

NGOME ya Vijana ya Chama cha ACT-Wazalendo, imelalamikia kitendo cha aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jecha Salim Jecha, kuchukua fomu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya kuomba uteuzi wa kugombea urais wa Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana ya chama hicho, Abdul Nondo, alidai kuwa kitendo cha Jecha aliyekuwa Mtendaji wa juu kabisa wa tume hiyo kuchukua fomu ni uthibitisho kuwa Mwenyekiti wa chama chao, Maalim Seif Sharif Hamad, hakutendewa haki katika uchaguzi wa mwaka 2015.

Maalim Seif wakati ule alikuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF).

"Kitendo cha aliyekuwa Mwenyekiti wa tume ya uchaguzi Zanzibar kuchukua fomu kimeidhihirishia dunia kuwa Maalim Seif alishinda uchaguzi wa mwaka 2015 ila hakutendewa haki," alidai Nondo.

Ngome hiyo imetaka mabadiliko katika tume ya uchaguzi ili kupata tume huru ya uchaguzi kama ambavyo imekuwa ikiliiliwa na vyama vya upinzani na wadau mbalimbali wa uchaguzi nchini ikiwamo asasi za kiraia ili kuwa na uchaguzi huru na wa haki.

Jecha Salim Jecha juzo alichukua fomu ya kugombea urais wa Zanzibar, akiwa ni mojawapo kati ya makada 15 waliokwishachukua fomu ya kuwania urais Zanzibar Baadhi ya makada wengine waliochukua fomu ni Waziri wa Ulinzi wa Tanzania, Dr.Hussein Mwinyi , Waziri wa Maji Prof. Makame Mbarawa na Shamsi Vuai Nahodha. Katika uchaguzi wa mwaka 2015 matokeo ya urais yalitenguliwa muda mfupi baada ya Maalim Seif aliyekuwa mgombea kupitia CUF kujitangazia ushindi jambo lililopingwa vikali na wadau mbalimbali wa uchaguzi.

Pamoja na upinzani na badhi ya wadau wa uchaguzi kuhusu uhalali wa kutenguliwa kwa matokeo hayo uchaguzi huo ulirudiwa katika awamu ya pili ya uchaguzi ambao hata hivyo ulisusiwa na baadhi ya vyama vya upinzani ikiwamo CUF na hatimaye Dk. Mohamed Shein kutangazwa mshindi katika nafasi ya urais.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiwapungia wananchi wakati alipowasili kwenye uwanja wa ndege wa Nachingwea akiwa njiani kwenda Ruangwa kwa ziara ya kikazi jana. Wa pili kushoto ni mkewe Mary na kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**.

# Wazee wampongeza JPM kwa kuwaboreshea makazi

Na Mwandishi wetu, MOROGORO

WAZEE wanaoishi katika Kituo cha Makazi ya wazee wasiojiweza cha Fungafunga mkoani Morogoro, wamempongeza Rais John Magufuli kwa kuwaboreshea makazi yao na huduma.

Wamesema uboreshaji kwa huduma za afya na makazi yao umesaidia kuishi katika mazingira rafiki.

Waliyasema hayo mbele ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii), Dk. John Jingu, alipofanya ziara kituoni hapo ya kukagua uendeshaji na huduma zinazotolewa kwa wazee.

Mmoja wa wazee hao, Joseph Kaniki, alisema serikali chini ya Rais Magufuli imewaboreshea huduma na kwamba afya zao zimeimarika ikilinganishwa na kipindi kilichopita.

"Kama unavyoona tunanawiri hivi ni kwa sababu tunatunzwa na tunakula vizuri, Mwenyezi Mungu azidi kuwalinda na kuwatunza Rais wetu, mawaziri, wewe Katibu wetu unayetutembelea kila mara pamoja na mama yetu mlezi," alisema Kaniki.

Naye, Mzee Abdallah Mbena, maarufu kama Chalinze, alisisitiza kuwa, wazee waishio katika vituo hivyo watakumbwa na kifo kwa mipango ya Mungu lakini siyo kwa kukosa huduma za kijamii.

Akitoa maelezo ya uendeshaji wa kituo hicho, Ofisa Mfawidhi wa Kituo hicho, Rehema Kombe, aliipongeza serikali kwa kuwajali na kuwatunza wazee huku akifafanua makazi hayo ni nyumbani na siyo mabweni kama ilivyotafsiriwa na wengi.

Aliongeza kuwa, makazi hayo yanahitaji kuboreshwa zaidi kwa kujengewa bwalo la chakula, ukarabati wa jiko na majengo mbalimbali yanayotumika kwa miradi inayoendelea kwenye makazi hayo.

Mkuu Dk. Jingu alisema: "Nyie mmefanya kazi, mnalima na nimeona Bustani, mchicha umestawi vizuri kabisa. Vijana wanaoshinda bila kazi wanatakiwa kuinga mfano kwenu".

Alisema serikali itaendelea kutoa huduma za chakula, mavazi, malazi na matibabu kwa wazee wasiojiweza

# Mbaroni wa tuhuma za kusafirisha bangi

Na Said Hamdani, LINDI

JESHI la Polisi mkoani Lindi,limemkamata na kumfikisha mahakamani mkazi wa eneo la Kata ya Mingoyo, Manispaa ya Lindi na Tandaimba, Mtwara, Yusufu Seph, kwa madai ya kukutwa akimiliki kinyume cha Sheria kilo 9 na gramu 200 za dawa za kulevya aina ya bangi.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoani humo, ACP Stanley Kulyamo, Yusufu alikamatwa na askari waliopo kizuio kilichopo eneo la SiDO katika Manispaa ya Lindi Juni 18, mwaka huu.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa na dawa hizo zenye uzito wa kilogram 9 na gram 200 zikiwa katika mifuko mitano ya plastiki na kuhifadhiwa kwenye begi rangi nyeusi la nguo.

Kulyamo alisema mtuhumiwa alikuwa anasafirisha bangi hiyo kwenye basi la abiria linalofanya safari zake kati ya wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi na jijini Dar es salaam.

Alisema Basi hilo lilipofika eneo hilo la kizuio, askari waliokuwapo kazini walilisimamisha na walipolifanyia ukaguzi walifanikiwa kukuta bangi hiyo, ikiwa ndani ya buti la basi husika.

Pia, alisema kubainika kwa mtuhumiwa Yusufu kulitokana na utaratibu uliobuniwa na mmiliki wa mabasi hayo kwa kuandika kwenye mizigo namba ya kiti kwenye tiketi ya abiria husika.

"Utaratibu huu ndio uliotuwezesha kumtambua mtuhumiwa badala ya kumbana kondakta wa basi husika," lisema Kamanda Kulyamo.

# AN-NAHC Trust yakabidhi vifaa tiba

Na Beatrice Shayo

TAASISI isiyo ya kiserikali ya AN-NAHC Trust kwa kushirikiana na Nama Foundation, imekabidhi msaada wa vifaa tiba na dawa vyenye thamani ya Sh. milioni 435.84 kwa serikali.

Mratibu wa Taasisi huyo, Hamza Jabir, akizungimza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki baada ya kukabidhi msaada huo, alisema mchango huo ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Jabir amesema kazi yao kubwa ni kuwa karibu na jamii, hivyo waliona kutakuwa na changamoto ya vifaa tiba katika vituo vya afya na kuamua kusaidia serikali.

Alisema vifaa hivyo wamevinunua katika Bohari ya Madawa (MSD) vina ubora unaotakiwa na wataendelea kuunga mkono jitihada za afya ili huduma ziendelee kuimarika kwenye vituo vya afya.

Aidha, Jabir amesema taasisi hiyo ilitenga Sh. bilioni 1.3 kwa kipindi hiki ambacho kulijitokeza changamoto mbalimbali kwa Tanzania katika masuala ya afya.

# Taasisi yasaidia vitabu wilaya 15

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

TAASISI ya Uwezo Tanzania imetoa vitabu vya kujifunza kusoma na kuandika kwa wanafunzi wanaojifunza kuanzia darasa la darasa la awali hadi la tatu katika wilaya 15 nchini.

Vitabu hivyo vilikabidhiwa juzi na Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Zaida Mgala kwa Ofisa Elimu Taaluma wa Wilaya ya Kisarawe, Zipporah Simwanza kwa niaba ya wilaya zingine.

Zaida alisema taasisi hiyo imebaini uwapo wa wanafunzi wengi wanaotumia muda mrefu kujifunza kusoma na kuandika, hivyo wamekuja na vitabu vya hadithi na simuulizi ambazo ni rahisi kwa watoto kujua kusoma haraka.

Alisema taasisi yao imefanya utafiti kuanzia mwaka 2011 hadi 2019 na kubaini wapo watoto katika shule mbalimbali ambao bado wanahangaika kujifunza kusoma na kuandika jambo lililowasukuma kubuni mbinu ya kuwa na vitabu vya hadithi vitakavyowavutia ambavyo pia itakuwa rahisi kwa wazazi kuwafundisha.

Simwanza aliishukuru Taasisi hiyo kwa kuikumbuka Wilaya ya Kisarawe katika kuhakikisha wanafunzi wanapata mbinu mbalimbali za kuwasaidia kujua kusoma kwa njia rahisi.

"Kupitia Taasisi hii ya Uwezo Tanzania watawezesha watoto wengi kujifunza kusoma na kuandika hata wakiwa nyumbani kwao kwa msaada wa wazazi wao, hivyo tutajitahidi kuhakikisha vinawafikia walengwa kwa wakati"

Taasisi ya Uwezo inashirikiana na Taasisi ya Champion Chanzige ambao ndio wanatekeleza mradi katika shule tano za msingi ambazo ni Marimbike, Manarumango, Kidugalo, Mtakano na Mitegwa katika Wilaya ya Kisarawe.

Ofisa mradi wa Chanzige, Gega Bujeje, alisema katika shule hizo tano kulifanyika utafiti kwa watoto 1,200 na kubaini watoto zaidi ya 235 hajui kusoma na kuandika, hivyo Taasisi hiyo iliweka mkakati wa kuwagawa watoto hao katika makundi kwa kipindi cha mwezi mmoja kwa lengo la kuwafuatilia kwa karibu.

# TAKUKURU yaokoa mil. 46/- za walimu 2 waliotapeliwa

**Na Dotto Mwaibale,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Singida, imefanikiwa kuokoa Sh. 46,500,000 za pensheni za walimu wawili walizodaiwa kudhulumiwa na mkopeshaji haramu.

Walimu hao waliodhulumiwa ni Loth Mwangu ambaye alikuwa anafundisha katika Shule ya Msingi Ilonga na Seleman Tyea ambaye alikuwa anafundisha katika Shule ya Msingi Endasiku zote za Wilaya ya Mkalama mkoani hapa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi fedha hizo kwenye ufunguzi wa mafunzo ya kupinga rushwa ya ngono kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu mkoani hapa kwa walimu hao ambazo walikabidhiwa na Mkuu wa mkoa huo, Dk. Rehema Nchimbi, Mkuu wa TAKUKURU wa mkoa huo, Adili Elinipenda, alisema taasisi hiyo Wilaya ya Mkalama ilipokea malalamiko kutoka kwa walimu hao wastaafu waliokuwa wakilalamikia kudhulumiwa fedha zao za pensheni na mkopeshaji aliyejulikana kwa jina moja la Bhoke kupitia mikopo umiza.

Alisema Mwalimu L Mwangu alistaafu Julai 15, mwaka 2016, baada ya kustaafu alianza kukopa fedha kutoka kwa mkopeshaji huyo na kufikia jumla ya Sh. milioni 9 kwa makubaliano ya kulipa kupitia fedha za pensheni atakazolipwa na fedha hizo alikuwa akikopa kidogo kidogo kuanzia Julai hadi Desemba mwaka 2016.

Elinipenda alifafanua kuwa pensheni ya mwalimu huyo ilipotoka, mkopeshaji huyo alimweleza mstaafu huyo kuwa anamdai Sh. 22,500,000 kutokana na mkopo sawa na riba ya asilimia 215.

Naye Mwalimu Seleman Tyea alikopa Sh. 2,000,000kutoka kwa mkopeshaji huyo huyo kwa makubaliano ya kulipa kupitia fedha za pensheni ambazo alizikopa kuanzia Mei hadi Desemba mwaka 2016 ambapo alistaafu Mei 16, mwaka 2016.

Baada ya pensheni mkopeshaji alimtaka mwalimu huyo kulipa Sh. 24,000,000 (sawa na riba ya asilimia 1,200), ambapo na mkopeshaji huyo alifanikiwa kumlipisha kiasi hicho kupitia Benki ya NMB Tawi la Singida.

Akizungumza baada ya kuwakabidhi fedha hizo, Dk. Nchimbi aliwataka wakopeshaji haramu mkoani hapa kujisalimisha na wasipofanya hivyo mkono wa TAKUKURU na dola utawakuta na hawatasalimika, na kwamba ni heri wajisalimishe kuliko kuwafuata huko waliko.



Mkuu wa Mkoa wa Singida Dk. Rehema Nchimbi (kushoto)akimkabidhi juzi Sh. 24,000,000/= Mwalimu Seleman Tyea zilizookolewa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Singida baada ya kudaiwa kudhulumiwa na mkopeshaji haramu. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**

# NMB yasaidia elimu, afya kwa mil. 200/-

**Na Mwandishi wetu,** SIngida

BENKI ya NMB imetoa msaada wa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200 katika wilaya kadhaa nchini.

Misaada iliyotolewa na benki hiyo ndani ya miezi mitano mwaka huu, inahusisha vifaa vya ujenzi, madawati na vifaa vingine vinavyowezesha ukamilishaji wa miradi ya afya, elimu na usalama wa raia.

Imeshatoa msaada wa vifaa vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200 kwa mikoa ya Kanda ya Kati.

Akifafanua kuhusu misaada hiyo wakati akikabidhi msaada wa madawati na vitanda kwa baadhi ya shule katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba mkoani Singida, Meneja wa Kanda ya Kati wa NMB, Nsolo Mlozi, alibainisha kuwa, misaada hiyo imelenga sekta ya elimu, afya na majanga kwa mikoa mitatu ya Kanda ya Kati.

Akikabidhi msaada wa madawati na vitanda kwa baadhi ya shule za Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, mkoani Singida, katika Shule ya Sekondari ya New Kiomboi, Mlozi alisema fedha hizo zilizotolewa na NMB zimetumika kununua madawati, viti vya shule za sekondari,vitanda na vifaa tiba kwenye sekta ya afya.

Aidha, alisema lengo la msaada hiyo ni kuunga mkono juhudi za serikali kuwahudumia wananchi kwenye sekta mbalimbali.

Pia alisema misaada hiyo imekabidhiwa kwa baadhi ya shule, zahanati, hospitali katika mikoa ya Singida, Dodoma na Manyara.

Pia NMB walikabidhi madawati 250 na vitanda 80 vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 29.5 kwa baadhi ya shule za wilaya ya Iramba mkoani humo.

Katika hatua nyingine, Benki hiyo imevipatia kituo cha Polisi wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro pamoja na Shule ya Msingi Msowelo mabati 160 yenye thamani ya Sh. milioni 5 kwa ajili ya kuezekea maboma.

Meneja wa NMB Kanda ya Mashariki, Baraka Ladislaus, alisema waliamua kutoa msaada huo ukiwa mpango wa kuzipunguza baadhi ya changamoto kwa taasisi za serikali nchini.

Baraka alisema kati ya mabati hayo, kituo cha polisi wilaya kimepa mabati 80, huku Shule ya Msingi Msowelo nayo ikipata idadi hiyo. Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kilosa, Mayenga Mapalala, alisema msaada huo utasaidia kumalizia ujenzi wa majengo ya kuhifadhi silaha na mahabusu.

Naye Ofisa Elimu ya Msingi Wilaya ya Kilosa, Christina Hauli, alisema mabati yaliyokabidhiwa kwa Shule ya Msingi Msowelo yatasaidia kumalizia ujenzi wa vyumba vya madarasa na kupunguza adha ya watoto kurundikana darasani.

Wakati huo huo, wakazi zaidi ya 6, 000 wa kijiji cha Nsola, wilaya ya Magu mkoani Mwanza wamepata matumaini ya kuondokana na adha ya kutembea umbali wa kilimita 11 kufuata huduma ya afya kijiji jirani cha Bubinza, baada ya Benki ya NMB kuwapatia vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 20 vitakavyotumika kukamilisha ujenzi wa zahanati kijijini hapo.

Pamoja na vifaa hivyo vilivyokabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Magu, Philemon Sengati, Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Donatus Richard, alisema benki hiyo pia imechangia madawati 130 yenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya shule za msingi za Matela na Muda wilayani humo na hivyo kufanya misaada yote kuwa na thamani ya Sh. milioni 30.

## HABARI KITAIFA

# Waziri ahakikishia kiwanda mali zilizozuiliwa bandarini

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amekihakikishia kiwanda cha Ocean Aluminium Ltd cha jijini Dar es Salaam kwamba kitapata zaidi ya tani 40 za aluminium, ambazo zimezuiliwa katika Bandari ya Dar es Salaam lakini baada ya wataalamu kujiridhisha kwamba bidhaa hiyo ni halali kuingia nchini. Kujiridhisha huko ni kwa mujibu sheria za kuingiza malighafi nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki jijini baada ya kutembelea kiwanda hicho, Zungu alisema serikali inaweka mazingira mazuri ya uwekezaji na kufanya biashara na haitaki kuwakatisha tama wawekezaji.

"Kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa aluminium hapa nchini na kiwanda kimeagiza shehena ya malighafi ambayo imekwama bandarini kutokana na sheria za usafirishaji wa taka hatarishi kutoka nje ya nchi, tutakaa na mamlaka zinazohusika na kupitia mikataba ya kimataifa ambayo tumeiridhia na kusaini ili kuona namna ambavyo kiwanda kinaweza kunufaika," alisema Waziri Zungu.

Alisema wakati huu ambapo taifa linatekeleza azma ya ujenzi wa viwanda, serikali inashughulikia changamoto mbali mbali ili kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji.

"Kiwanda hiki kinalipa kodi zaidi ya shilingi bilioni 1.2 na kimeajiri wafanyakazi zaidi ya 100, tutachukua hatua ambazo pande zote zitanufaika hasa baada ya kufanya ukaguzi wa mzigo ulioagizwa kwa kutumia wataalamu wetu na tukijiridhisha basi mzigo huo wa tani zaidi ya 40 utafika kiwandani ili kuendelea na uzalishaji," alieleza Zungu.

Aidha amewataka wafanyabiashara kufuata taratibu zinazotakiwa kupitia taasisi zinazohusika ikiwemo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), hasa wanaoingiza taka hatarishi kutoka nje ya nchi.

"Kiwanda kimeagiza shehena za malighafi kutoka nje ya nchi na NEMC haikushirikishwa., hivyo natoa wito kwa wafanyabiashara wanaotumia malighafi za taka hatarishi kama aluminium kuwasiliana na mamlaka zinazohusika kwani zipo sheria zinazozuia usafirishaji wa taka hatarishi."

Meneja Uajiri wa kiwanda hicho, Aisha Omary, alisema ujio wa waziri kiwandani hapo utasaidia katika kushughulikia changamoto za ukosefu wa malighafi ya kutosha katika uzalishaji.

"Kiwanda kimeanza uzalishaji mwezi wa kwanza mwaka huu, lakini tumekuwa na changamoto ya upatikanji wa malighafi. Tunaamini ujio wa Waziri utasaidia upatikanji wa tani zaidi ya 40 ambazo ni malighafi muhimu kwa utengenezaji wa sufuria," alisema Aisha, na kuongeza kwamba kiwanda kitashirikiana na NEMC pamoja na taasisi zote zinazohusika ili kukidhi matakwa ya kikanuni na sheria za ndani na mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania imeiridhia.




Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akizungumza na wadau wa sheria na haki za binadamu (hawapo pichani), alipokuwa akifunga mkutano wa majadiliano ya kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kupata Katiba Mpya mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. Kulia ni mwezeshaji katika majadiliano hayo, Dk. Leonce Mujwahuzi. **PICHA: MBARAKA KAMBONA.**

# Wanakijiji waishukuru SBL kwa mradi wa maji

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa vijiji vya Galangal na Gidagamowd mkoani Manyara, wameishukuru Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kwa kufadhili mradi wa maji utakaowawezesha vijiji hivyo viwili kupata huduma ya majisafi na salama.

Ukiwa na uwezo wa kuzalisha lita 156,000 kwa siku, mradi huo ni sehemu ya utaratibu wa kumpuni ya SBL kusaidia jamii zinazoishi katika sehemu zenye changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji kupata huduma hiyo kupitia mradi wake unaojulikana kama "Maji ni Uhai"

Jeremiah Mathiya, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Gidagamowd, alisema maisha ya wananchi katika kijiji chake yatabadilika kwa kiasi kikubwa kutokana na upatikana wa huduma hiyo muhimu.

"Kabla ya kuwapo kwa mradi huu watu walikuwa wakiugua magonjwa mbalimbali ya tumbo kutokana na kutumia maji yasiyo safi na salama. Kutokana na mradi huu afya za watu zitaimarika na pia watapata muda mwingi zaidi wa kufanya kazi kwa kuwa hawatalazimika kutembea umbali mrefu kutafuta maji, tunaishukuru sana kampuni ya SBL," alisema.

Mariam Desiri, mkazi wa Kijiji cha Gidagamowd, alisema kwa kipindi kirefu wakazi wa Kijiji hicho wamekuwa wakilazimika kutumia maji ya mvua yaliyotuama ambayo siyo salama kiafya.

"Kabla ya mradi huu tulilazimika kutumia maji ya mvua yaliyotuama ambayo pia wanyama walikuwa wakiyatumia. Ili kupata maji ya kunywa tulilazimika kutembea zaidi ya kilomita 15 kwenda kata ya Vindadi. Mradi huu ulioletwa na kampuni ya SBL ni ukombozi mkubwa sana haswa kwa sisi kinamama ambao ndiyo tulikuwa tunabeba mzigo wa kutafuta maji," alisema.

Mkazi mwingine wa Kijiji hicho, Askadi Dodaye, alisema mradi huo pia unatoa nafasi kwa wanafunzi kuhudhuria masomo yao bila kukosa kwa kuwa kabla ya kuwapo wakati mwingine walilazimika kuacha kwenda shule na kuwasaidia wazazi wao kutafuta maji.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Mahusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, zaidi ya Watanzania milioni moja wamenufaika kupitia mradi wa "Maji ni Uhai" katika kipindi cha miaka 10 iliyopita.

"Tumetekeleza mradi wa aina hii katika mikoa mingine ikiwamo Iringa, Kilimanjaro, Mwanza, Tanga, Ruvuma, Dar es Salaam, Pwani na Dodoma. Miradi hii imeweza kubadilisha maisha ya jamii ambazo zinaishi katika sehemu zenye uhaba mkubwa ya huduma ya maji safi na salama," alisema Wanyancha.

# Sri Lanka yaishukuru Tanzania ushirikiano kurejesha raia wake

**Na Romana Mallya**

UBALOZI wa Heshima wa Sri Lanka nchini, umeishukuru Tanzania kwa ushirikiano uliowapatia katika kufanikisha kuratibu urejeshaji wa raia wake 149 waliokuwa wamekwama hapa na nchi za jirani kwa kipindi cha miezi minne.

Akizungumza na waandishi wa habari Jumamosi katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Balozi Mdogo wa Sri Lanka nchini, Hiran Sumanaweera, alisema wananchi wao waliokuwa wamekwama Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Zambia kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania wamefanikiwa kuwasafirisha siku hiyo kurejea makwao.

"Raia hawa wataungana na wenzao wapatao 142 kutoka nchi ya Madagascar hivyo kufanya idadi yao kwa ujumla kufikia 291 ya raia wanaorudi Sri Lanka baada ya kukwama kwa muda katika nchi hizo tofauti, watatumia ndege ya Shirika la Ndege la Sri Lanka yenye usajili namba UL1709," alisema.

Alisema raia hao walikwama kwenye nchi hizo kwa sababu mbalimbali ikiwamo zuio la safari lililotokana na ugonjwa wa virusi vya corona ulioikumba dunia.

"Wananchi hawa walikuja kwenye nchi hizo kwa sababu mbalimbali, wapo waliokuja kusalimia familia zao, biashara pamoja na utalii.

"Tunaishukuru serikali ya Tanzania kwa ushirikiano walioutoa kwetu kwa kufanikisha raia hawa waliokuwa wamekwama nchi tano kukusanyika jijini Dar es Salaam na kuondoka leo (Jumamosi) saa tisa alasiri kupitia uwanja huu wa Kimataifa wa ndege wa Julius Nyerere terminal 3."

Aliishukuru Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya nje ya Sri Lanka, Rais wa Sekretarieti ya nchi hiyo, na Balozi zote za nchi husika ambazo raia wao walikwama.

Meneja Mradi ujulikanao kama Bukinda Hydropower unaotekelezwa nchini Uganda, Mohammed Mafas, ambaye ni miongoni mwa waliokuwa wamekwama aliishukuru Uganda na Tanzania kwa ushirikiano walioufanya kuhakikisha wanarejea makwao.

Nahodha wa ndege hiyo, Nuwan Gunaratne, alisema Tanzania ni marafiki na nchi yao, na kwamba wapo wa Sri Lanka wengi wanaofanya kazi hapa na nchi nyingine za Afrika.

# Nipashe Spotika



USAJILI 10 GHALI ZAIDI CHELSEA UK. 12&13



# RONALDO, SARRI KATIKA VITA MPYA JUVENTUS

**TURIN, Italia**

BAADA ya Juventus kufungwa na Napoli kwenye fainali ya Coppa Italia, kocha wake, Maurizio Sarri, alisema Cristiano Ronaldo na nyota wengine wa timu hiyo hawana makali.

Wachezaji hao wamekosa ufiti baada ya kurudi dimbani wakitoka kwenye "likizo" ya miezi mitatu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Sarri alibainisha wachezaji wake hao hawakucheza kwa kiwango chao na kusababisha kufungwa kwenye fainali hiyo na kulikosa kombe hilo la Italia.

Na Ronaldo ndio ameonekana kuangushiwa jumba bovu kutokana na kupoteza fainali hiyo kwa mikwaju ya penalti 4-2.

Awali, ilionekana kama Juventus inakwenda kubeba taji hilo, lakini ghafla Napoli inayonolewa na kocha, Gennaro Gattuso ikakomaa na kupindua meza kwenye mikwaju ya penalti.

Hata hivyo, baada ya mchezo huo Sarri akasema kuwa supastaa wake Ronaldo hakuwa kwenye ubora na hakupambana kuhakikisha taji hilo linakwenda Turin.

Lakini, katika kile kinachoonekana kuibuka kwa vita ya maneno, dada wa Ronaldo, Katia Aviero, ameibuka na kuelekeza lawama kwa Sarri akisema, ndiye anayepaswa kulaumiwa na sio kaka yake.

Tangu kurejea kwa soka la Italia baada ya kusimama kutokana na corona, Juventus haijaonekana kucheza kwenye ubora wake, ikianza kwa sare ya bila kufungana kwenye mechi ya ligi na juzi Jumatano ikalazimishwa sare na Napoli kwenye fainali hiyo kabla ya kuchapwa kwa matuta.

Katika mchezo huo wa fainali, Ronaldo hakuwahi kupiga penalti yake ya mwisho kwani Napoli walishamaliza mchezo.

Waliotangulia kupiga penalti za Juve ni Paulo Dybala na Danilo ambao walikosa penalti zao, wakati Leonardo Bonucci na Aaron Ramsey walifunga.

Hii ni mara ya kwanza kwa Ronaldo kupoteza mchezo wa fainali mara mbili mfululizo katika miaka yake 18 ya kucheza soka la kulipwa.

Katika fainali iliyotangulia akiwa na Juventus kwenye Super Coppa Italiana walichapwa na Lazio mwishoni mwa mwaka jana.

Hata hivyo, dada yake, Katia anaamini kuwa mbinu za Sarri ndio zimeimaliza Juventus kutokana na kuingia na mfumo wa kujilinda hivyo, kutompa fursa Ronaldo kupata mipira akiwa eneo la adui.

"Kitu gani zaidi unaweza kufanya, mlitaka afanye miujiza kuiokoa timu peke yake? Mbinu za mwalimu ndio zimeiua Juve na sio Ronaldo," aliandika Katia kupitia ukurasa wake wa Instagram.

Sarri, ambaye alifutwa kazi Chelsea, alifunguka kuwa alivurugwa na matokeo hayo, lakini ameshtushwa na kiwango cha chini cha Ronaldo katika mchezo huo.

"Sikuwa na mengi ya kusema kwa wachezaji wangu baada ya mchezo, nilikuwa na hasira na nimeshtushwa na ubora wao. Kwa wakati huu ni muhimu kukaa kimya," alisema Sarri.

Lakini sasa kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Italia, hali inavyoonekana ndani ya kikosi hicho kuna uwezekano mkubwa wa kati ya Ronaldo au Sarri mmoja wao akaonyeshwa mlango wa kutokea.

Bado viongozi wa klabu hiyo hawajatoa kauli yoyote, lakini inaonekana wazi kwamba, kuna uwezekano mkubwa sana wa mmoja wao kuondoka klabuni hapo.


Hivi karibuni mchezaji mwenzake na Ronaldo katika Timu ya Taifa ya Ureno, Nani, alibainisha kwamba, anaamini nyota huyo ataungana nae nchini Marekani kumalizia soka lake.

Sasa kwa hali inavyokwenda ndani ya Juventus ni wazi kwamba maisha ya Ronaldo ndani ya kibibi kizee hicho cha Turini yanaweza kufikia mwisho na nyota huyo akaamua kuondoka zake.

Inawezekana dirisha la usajili wa kipindi hiki cha majira ya joto likifunguliwa kuwa na mambo mengi zaidi.

## ISIKUPITE

Wakati msimu wa mwaka 2019/20 ukielekea ukingoni, mshambuliaji wa Real Madrid, Karim Benzema amecheza dakika 4768, akifunga mabao 25 katika mechi 39 za mashindano mbalimbali alizocheza msimu huu. Huu ni msimu wake wa 11 ndani ya Madrid ambayo ameitumikia katika michezo 530 na kuzifumania nyavu mara 243.



NIPASHE JUMATATU JUNI 22, 2020







# USAJILI 10 GHALI ZAIDI CHELSEA

**LONDON, England**

CHELSEA ina historia ya kutoa fedha nyingi kwenye usajili (kuanzia mwaka 2003), na baada ya kumaliza adhabu ya kufungiwa kutofanya usajili, Blues hao wamerudi tena sokoni.

Timu hiyo yenye maskani yake jijini London imekamilisha usajili wa straika wa RB Leipzig aliyekuwa akiwindwa sana na Liverpool, Timo Werner kwa pauni milioni 47.5 - akiwa ni mchezaji wa sita ghali zaidi katika historia ya usajili wa Chelsea.

Makala hii inakuchambulia wachezaji 10 ghali zaidi kusajiliwa na Chelsea .

**10. Michy Batshuayi - pauni milioni 35.1**

Batshuayi ulikuwa usajili wa kwanza wa Kocha , Antonio Conte, wakati alipomnunua straika huyo wa Ubelgiji kutoka Marseille ya Ufaransa mwaka 2016.

Hata hivyo, alishindwa kuthibitisha ubora wake, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 akitumia muda mwingi kucheza kwa mkopo nje ya Stamford Bridge. Amefunga mabao nane tu kwenye Ligi Kuu England.

9. Tiemoué Bakayoko - pauni milioni 36

Bakayoko alitumia msimu mmoja kucheza Chelsea mara baada ya kusajiliwa kutoka kwa waliokuwa mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Monaco, dili ambalo wakati huo lilifanya kuwa usajili ghali wa pili wa wakati wote ndani ya klabu hiyo.

Hata hivyo, baada ya kuanza na msimu vibaya alikumbwa na mikasa zaidi kwa kutolewa nje ndani ya dakika 30 kwenye mchezo dhidi ya Watford na akapelekwa kwa mkopo kule Milan na Kocha, Maurizio Sarri.

Na hakuwa pia na wakati mzuri kwa miamba hao wa Serie A na Bakayoko akatumia msimu 2019/20 akicheza kwa mkopo Monaco.

**8.Hakim Ziyech - pauni milioni 36**

Kijana huyu aliyekulia Ajax alionyesha kiwango cha kuvutia zaidi wakati timu hiyo ikitinga nusu faiali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na Chelsea wakaamua kumchukua na walishamalizana na klabu yake tangu Feburari.

Winga huyo mwenye kasi ya ajabu aliwapeleka puta Chelsea kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya alipotoa pasi za mwisho tatu wakati mchezo ukimalizika kwa sare ya 4-4 baina ya timu hizo.

Ziyech ambaye atajiunga na Chelsea kipindi hiki cha majira ya joto ametoa pasi za mwisho 82 katika mechi 165 kwa Ajax, na sasa atatakiwa kuthibirisha ubora wake kwa miamba hao wa Ligi Kuu England.

7. Andriy Shevchenko - pauni milioni 39

Jose Mourinho alivunja rekodi ya usajili kwenye soka la Uingereza wakati alipomsajili Shevchenko kutoka AC Milan mwaka 2006.

Ilikuwa ni ndoto ngumu, kwani Shevchenko alikuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani na mfungaji wa pili wa wakati wote wa Milan, na mshindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ballon d'Or.

Hata hivyo, mambo yanakwenda kama yalivyotarajiwa. Straika huyo alifunga mabao manne tu kwa msimu wote. Hakuwekwa hata benchi kwenye mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Chelsea ikicheza na Liverpool.

Msimu uliofuata, Shevchenko alirudishwa kwa mkopo Milan, kabla ya kwenda kucheza katika klabu yake ya utotoni ya Dynamo Kiev mwaka mmoja baadaye.

**6.Mateo Kovacic - pauni milioni 40.5**

Kovacic awali alijiunga na Chelsea kwa mkopo kutoka Real Madrid mwaka 2018, kabla ya kusajiliwa moja kwa moja kipindi cha majira ya joto.

Hakuwa na namba ya kudumu katika kikosi cha kwanza cha Blues hao katika msimu wake wa kwanza wa Ligi Kuu England chini ya kocha, Maurizio Sarri, lakini kiungo huyo amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu kwa kikosi hicho msimu huu.

Kovacic amerudi kwenye ubora wake chini ya Frank Lampard, amejiimarisha yeye mwenyewe chini ya kocha huyo mpya kama mmoja wa wachezaji bora zaidi.

**5. Fernando Torres - pauni milioni 50**

Fowadi huyu alivunja mioyo ya mashabiki wa Liverpool wakati alipokamilisha usajili wake siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili na kutua Chelsea Januari 2011, na akaenda kucheza dakika 903 bila kufunga bao kabla ya kufunga bao lake la kwanza kwa klabu hiyo, Aprili.

Torres hakuweza kuonyesha kiwango chake kama ilivyokuwa katika dimba la Anfield na alifunga mabao 38 katika kipindi cha miaka mitatu na nusu aliyokaa hapo Chelsea.

**4. Jorginho - pauni milioni 51**

Jorginho alikuwa na wakati mgumu kuzoea soka la England kutoka Napoli mwaka 2018. Kiungo huyo alimfuata kocha, Sarri kutoka Serie A na kutua hapo Stamford Bridge.

Alikuwa na wakati mzuri chini ya Sarri, akianza mara 37 kwenye Ligi Kuu msimu wa 2018/19, lakini aliendeleza ubora wake na amekuwa akitumika mara kwa mara chini ya Lampard.

Pia Jorginho amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka pale Stamford Bridge kipindi hiki cha majira ya joto, huku Sarri akitajwa kutaka kuungana nae kule Juventus.

**3. Christian Pulisic - pauni milioni 52**

Winga huyo alikuwa mchezaji ghali zaidi kwa soka la Marekani wakati aliposajiliwa kwa pauni milioni 52 kutoka Borussia Dortmund kwenda Chelsea Januari 2019.

Pulisic alitumia kipindi cha msimu kilichobaki kucheza kwa mkopo kule Dortmund, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 amekuwa na wakati mzuri katika mwaka wake wa kwanza nchini England.

Nyota huyo wa kimataifa wa Marekani aliingia kwenye kikosi cha kwanza cha kocha, Frank Lampard Oktoba, akifunga mabao matano, ikiwapo 'hat-trick' dhidi ya Watford. Majeruhi yamekuwa wakimwandama mara kwa mara, lakini ana nafasi ya kufanya vizuri zaidi hapo Stamford Bridge.

2.Alvaro Morata - pauni milioni 60

Chelsea ililipa pauni milioni 60 kwa Morata kumchukua kutoka Real Madrid mwaka 2017, huku straika huyo wa Hispania akitarajiwa kuwa nguzo muhimu kwa kikosi hicho.

Maisha yake nchini England alianza vizuri, akifunga bao kwenye mchezo wake wa kwanza na 'hat trick' Septemba. Kufika Desemba, Morata tayari alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia.

Hata hivyo, akaanza kuwa na ukame wa mabao na Januari 2019, baada ya mabao 24 kwenye mechi 72, Morata alipelekwa kwa mkopo kule Atletico Madrid, na akahamia moja kwa moja kipindi cha majira ya joto.

**1.Kepa Arrizabalaga - pauni milioni 72**

Thibaut Courtois alilazimisha usajili wa kwenda Real Madrid kipindi cha majira ya joto 2018, huku Chelsea ikivunja rekodi yake ya usajili na rekodi ya dunia kwa golikipa ili kupata mrithi wake kutoka Athletic Bilbao, Kepa Arrizabalaga. Alifurahia msimu wake wa kwanza pale Chelsea, akicheza mechi 14 bila kuruhusu bao kati ya mechi 26 za Ligi Kuu England, lakini aliingia kwenye mzozo baada ya kukataa kutolewa nje kwenye fainali ya Kombe la Ligi.

Kepa msimu wake wa pili pale Bridge haujawa wa kuvutia zaidi. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alitemwa Januari kutokana na kiwango kibovu, lakini alirudi kwenye ubora wake kabla ya mlipuko wa virusi vya corona.


Luka Modric

## Nukuu

"John Bocco (nahodha wa Simba), ni mtu safi, mpole na kiongozi imara. Anatuongoza katika njia nzuri na wakati wote anatuhamasisha katika kutafuta ushindi uwanjani,**" Meddie Kagere, mshambuliaji anayeongoza katika kupachika mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara alisema.**



"Ronaldo (Cristiano) ameisaidia Juventus kupiga hatua nyingine mbele, ametupa msukumo mkubwa, amemfanya kila mmoja wetu kuwa kwenye ubora wake na kuipa msukumo jamii yote, yeye ni wa daraja jingine kabisa, tunacheza kwa ajili yake na kumfanya awe na kiwango bora kabisa, **" nyota wa Juventus, Giorgio Chiellini, alisema alipokuwa akizungumza na Martina Colombari kwenye Instagram.**



"Nimekuwa nikiwaona Arsenal wakicheza hivi hivi kwa miaka 10. Hawako vizuri, kuna kazi kubwa kwa Mikel Arteta, walikuwa na tatizo la beki wa kati hata kabla Arteta, na bado tatizo hilo lipo," **Mchambuzi wa soka na beki wa zamani wa Liverpool, James Carragher, alisema baada ya timu hiyo kufungwa mabao 3-0 na Manchester City.**





Kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), kilichoshiriki katika mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka jana (AFCON 2019), ndani ya uongozi wa miaka mitano ya Rais John Pombe Magufuli.

# MICHEZO ILIVYOPAISHA MIAKA MITANO YA JPM

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni miaka mitano ya kusisimua katika tasnia ya michezo, chini ya uongozi wa Rais John Pombe Magufuli 'JPM'.

Ni miaka mitano ambayo Watanzania wapenda michezo hawataisahau, kwa sababu imekuja kuibua tena nchi ambayo kwa miaka kadhaa ilikuwa imelala au kusuasua kwenye masuala ya michezo.

Hata alipotoa hotuba yake ya kuvunja Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania siku ya Jumanne iliyopita, JPM ameitaja michezo, sanaa kuwa ni moja ya vitu ambavyo katika kipindi chake cha uongozi, iliipaisha kwa kiasi kikubwa bendera ya nchi katika mashindano ya kimataifa.

"Na kwa hilo, naipongeza sana timu yetu ya taifa ya soka ambayo baada ya takribani miaka 39 kupita, hatimaye mwaka jana 2019 ilifanikiwa kufuzu kuingia fainali ya Kombe la Afrika," alisema Bungeni.

Mbali na Stars, Rais pia aliwapongeza wanamichezo mbalimbali wa ngumi na riadha ambao kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita walipeperusha vema bendera ya taifa.

"Mheshimiwa Spika, kutokana na mchango mkubwa unaotolewa na wasanii na wanamichezo, serikali imejipanga katika miaka mitano ijayo kuweka mkazo mkubwa zaidi kwenye sekta hii iliyowaajiri vijana wetu wengi," aliahidi.

Kwenye makala hii, tunaangalia mafanikio ya michezo yote iliyopatikana nchini chini ya uongozi wa miaka mitano ya JPM.

**WANAWAKE KUTWAA CECAFA MARA MBILI**

Chini ya uongozi wa Rais Magufuli, Timu ya Taifa ya wanawake ya Tanzania Bara 'Kilimanjaro Queens' ilifanikiwa kutwaa Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) mara mbili.

Mara kwa kwanza ilikuwa ni mwaka mmoja tu baada ya utawala wake, mwaka 2016, ilipotwaa ubingwa huo nchini Uganda kwa kuifunga Kenya mabao 2-1 kwenye mechi ya fainali iliyochezwa mjini Jinja.

Yalikuwa ni mabao ya Mwanahamisi Omari 'Gaucho' na Stumai Abdallah.

Miaka miwili baadaye, timu hiyo ilifanikiwa kutetea kikombe hicho kwa kuifunga Timu ya Taifa ya Ethiopia mabao 4-1, Julai, mwaka 2018 Katika mashindano yaliyofanyika jijini Kigali, Rwanda.

Kabla ya hapo iliifumua Uganda mabao 4-1 na kutoka sare na Kenya kwa kufungana bao 1-1.

**SIMBU KUSHINDA MARATHON**

Baada ya muda mrefu tangu kupita, hatimaye Tanzania ilifanya vema kwenye riadha mwezi Januari, mwaka 2017, miaka miwili tu ya kutwaa madaraka Rais Magufuli, pale mwanariadha aliyekuwa mgeni masikioni mwa watu, Alphonce Simbu alipotwaa medali ya dhahabu katika mashindano ya riadha ya dunia yaliyojulikana kama Mumbai Marathon yaliyofanyika nchini India.

Alitumia saa mbili, dakika tisa na sekunde 32 kuipeperusha vema bendera ya Tanzania.

**MWAKINYO KUMTWANGA MWINGEREZA**

Ilikuwa ni Septemba, mwaka 2018, kwa bondia Mtanzania asiye na jina, Hassan Mwakinyo, alipoishangaza dunia alipomtwanga Mwingereza Sam Eggington nchini Uingereza, kwenye pambano la utangulizi la bondia Amir Khan dhidi ya Samuel Vargas.

Pambano hilo lililochezwa kwenye ukumbi wa Arena Birmingham, jijini Birmingham ndilo lililomtangaza Mwakinyo na kuhesabika kuwa mmoja wa mabondia bora kabisa kwa sasa nchini, baada ya kumtwanga bondia huyo ambaye ni bingwa wa zamani wa Uingereza, Ulaya na Jumuiya za Madola kwa (TKO) sekunde ya 45 raundi ya pili.

Baada ya pambano hilo, Mwakinyo alipata sifa na hivyo kuandaliwa pambano lingine nchini Tanzania ambalo alipigana dhidi ya mmoja wa mabondia maarufu kabisa duniani, Arnel Tinampay mwishoni mwa Novemba mwaka jana 2019.

Mwakinyo alidhihirisha kuwa hakubahatisha kwa kumfinyanga Mfilipino huyo kwa pointi na kuzidi kuipaisha nchi ndani ya utawala huu.

**SIMBA KUNG'ARA AFRIKA**

Simba ilifanikiwa kutinga hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mara kwanza tangu ilivyofanya hivyo mwaka 2003, baada ya miaka 15 kupita, wakati Tanzania ilipokuwa chini ya Uongozi wa Awamu ya Tatu ikiongozwa na Rais, Benjamin Mkapa.

Baada ya miaka hiyo kupita, chini ya Rais Magufuli, Simba ilifanikiwa kutinga hatua ya makundi baada ya kuichapa Nkana FC ya Zambia mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na kufanikiwa kutinga kwa jumla ya mabao 4-3, baada ya kufungwa mabao 2-1 nchini Zambia.

Mechi iliyosisimua wengi ilichezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini dhidi ya Nkana ambayo iliipeleka Simba hatua hiyo ilichezwa mwishoni mwa Desemba 2018.

Simba pia ilikuwa ndiyo timu ya mwisho kutinga hatua hiyo mwaka huo huo wa 2003.

Baada ya miaka 25, Simba ilifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuifunga AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kwa mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Taifa jijini, mechi iliyochezwa Machi mwaka jana.

Ingawa Simba iliwahi kufika nusu fainali ya michuano hiyo mwaka 1974, chini ya utawala wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, lakini pia ilifika robo fainali mwaka 1994, Tanzania ikiongozwa na Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili.

Rais Magufuli aliingia kwenye rekodi ya kuwa mmoja wa Marais ambao wametawala nchi, na klabu ya soka kufanikiwa kufika hatua hiyo.

**STARS KUTINGA AFCON**

Machi mwaka jana, Timu ya Taifa (Taifa Stars), ilikata tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kwa kuichapa Uganda mabao 3-0 na kushika nafasi ya pili kwenye Kundi L, ikimaliza kwa pointi nane, kundi likiongozwa na Uganda iliyokuwa na pointi 13.

Ni moja kati ya mafanikio makubwa kwenye michezo nchini Tanzania, chini ya serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Magufuli.

Ni kwa sababu mara ya mwisho Stars kufanya hivyo ilikuwa ni miaka 39, ilipoitoa Zambia kwa jumla ya mabao 2-1, ikishinda bao 1-0 nyumbani na kutoka sare ya bao 1-1 mjini Ndola mwaka 1979.

Wakati huo nchi ilikuwa kwenye uongozi wa Awamu ya Kwanza chini ya Mwalimu Nyerere na ikacheza fainali zake mwaka 1980 nchini Nigeria.

Vizazi kadhaa vilipita bila kuona tukio hilo, ambalo lilikuja kutokea tena kwenye Awamu ya Tano, Stars ikifuzu na kucheza fainali zake nchini Misri.

**WASICHANA KUTWAA COSAFA**

Mafanikio mengine ya michezo nchini chini ya uongozi wa Rais Magufuli ndani ya miaka yake mitano ni pale timu ya soka wa wanawake chini ya miaka 20 'Tanzanite' ilipofanikiwa kulichukua Kombe la Mataifa ya Kusini kwa Afrika (COSAFA).

Baada ya kufanya vema ma kutinga fainali, Tanzanite iliitwanga Zambia kwenye mechi ya fainali iliyochezwa Agosti, mwaka jana 2019 nchini Afrika Kusini kwa mabao ya Opa Clement na Protasia Mbunda.

**U-20 KUTWAA CECAFA**

Timu ya Taifa ya vijana ya Tanzania Bara chini ya miaka 20 nayo haikuwa nyuma, Oktoba mwaka jana 2019 ilitwaa Kombe la Afrika Mashariki na Kati kwa kuwafunga wenzao kutoka Kenya katika mechi ya fainali iliyofanyika kwenye Uwanja wa Njeru, Jinja nchini Uganda.

Rekodi zinaonyesha kuwa hiyo ilikuwa ni mara ya pili kutwaa. Mara ya kwanza ilikuwa mwaka 1971, chini ya uongozi wa Rais wa Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere na haikufanikiwa, hadi utawala huu wa Rais Magufuli.

**JE, WAJUA?**



Straika wa zamani wa Timu ya Taifa ya Cameroon, Samuel Eto'o, alitangaza kustaafu kucheza kabumbu mwaka 2014, akiwa amefunga mabao 56 katika mechi 118 alizoitumikia timu hiyo. Ni mshindi wa tuzo ya Mchezaji Bora wa Afrika mara nne.





# Skimu 384 kujengwa miaka mitano ijayo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC), inatarajia kujenga na ku-karabati skimu 384 zitakazogha-rimu kiasi cha Sh. bilioni 986.8, ili kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali nchini.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki jijini hapa na Mkuru-genzi Mkuu wa Tume hiyo, Daudi Kaali, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya sekta ya uwagiliaji kwa miaka mitano na mikakati ya miaka mitano ijayo.

Alisema skimu hizo zitajengwa kwa miaka mitano ijayo kwenye mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Tabora na Katavi na zitaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 400,491.8.

"Fedha hizo zitakazotumika zitatokana na programu ya kue-ndeleza sekta ya kilimo awamu ya pili (ASDP II) ambapo serikali itachangia asilimia 41 ya ghara-ma hizo sawa na Sh.bilioni 80.9 kwa mwaka," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema ujenzi na ukarabati huo wa miundombonu ya umwagiliaji utatumia utaratibu wa 'force ac-count' ili kuondokana na tatizo la ucheleshaji miradi na kupun-guza gharama za utekelezaji.

"Matarajio yetu ni kuhakikisha tija katika uzalishaji kwa mazao mbalimbali katika skimu zote za umwagiliaji nchini inaongezeka," alisema.

Kaali alisema hatua hiyo itaongeza mchango wa sekta hiyo katika uhakika wa chakula nchini kutoka asilimia 24 ya sasa hadi asilimia 30 ya mahitaji yote ya chakula ifikapo mwaka 2025.

Pamoja na mikakati hiyo, Mkurugenzi huyo alisema kuna tatizo la uhaba wa fedha za kutekeleza shughuli za umwagil-iaji ambapo fedha zinazotengwa ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi na pia wakati mwingine hazitoki kwa wakati.

Aidha alisema katika msimu wa mwaka 2019/20, skimu 40 zilipata athari ya mafuriko na kwasasa Tume hiyo inaendelea kufanya tathmini ya uharibifu huo ili kujua gharama za ukara-bati wake.

"Pia Tume inakabiliwa na uhaba wa wataalam wa umwa-giliaji ambapo kuna watumishi 213 kati ya 438 wanaohitajika na hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 225,"alisema.

# Wakuu wa vyuo wapewa mbinu rushwa ya ngono

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKUU wa vyuo vya elimu ya juu nchini wametakiwa kuweka mikakati ya kuwafichua na kuwaondoa katika nafasi zao wahadhiri wanaoomba rushwa ya ngono kwa wanafunzi.

Rai hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dk. Binilith Mahenge, alipokuwa akifungua mafunzo ya kukabiliana na rushwa ya ngono kwa wanafunzi wa vyuo hivyo yaliyoandaliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na mikakati hiyo kwa kuwa wapo baadhi ya wahadhiri ambao hawafanyi kazi yao kwa uadilifu na wamekuwa wakiomba rushwa kwa wanafunzi ili kuwaongezea alama za ufaulu.

"Wakuu wa vyuo wekeni mikakati ya kuwabaini wahadhiri wanaoomba rushwa ya ngono kwa wanafunzi, mkiwagundua hao waiteni wawekeni pembeni, wachukueni vijana wengi wenye uwezo wa kufundisha," alisema.

Aliongeza: "Naamini wakiambiwa kuwa wenzao waliondolewa kwa sababu ya rushwa ngono, lazima watakuwa na hofu, hivyo hapatakuwa na walimu, wahadhiri, wala wataalamu watakaomba rushwa ya ngono wanafunzi."

Alisema kuwa licha ya kuweka mikakati ya kuwadhibiti wahadhiri, pia wanafunzi wanatakiwa kuwa waadilifu, kusoma kwa bidii na kuacha tabia ya kuwashawishi walimu wao kupokea rushwa ya ngono.

Mkuu huyo alisema wapo wanafunzi ambao hawasomi kwa bidii wakiamini kuwa hata wakifanya vibaya watawashawishi walimu kupokea rushwa ya ngono ili waongezewe ufaulu.

Aliitaka Takukuru kuwa na mawasiliano ya karibu na vyuo ili kukomesha rushwa ya ngono.

Awali, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema kuanzia mwaka 2013 hadi 2020, imepokea majalada 23 ya rushwa ambapo kati ya hayo, kesi 10 zilipelekwa mahakamani.

"Changamoto iliyopo ni kupata taarifa kuhusu rushwa ya ngono tumeona tutoe elimu ili kuelimishana, kujaribu kuhamasishana kuvunja ukimya na kutoa taarifa," alisema Kibwengo.

Kibwengo alisema ndoto za wanawake zimekuwa zikikatishwa na watu wachache kwa kuomba rushwa ya ngono.

Naye, Makamu Mkuu wa Chuo cha Mipango Dodoma, Dk. Proventi Dimoso, alisema mafunzo hayo yatawasaidia wanafunzi kuvunja ukimya na kupaza zauti zao dhidi a vitendo hivyo.



Mwenyekiti wa Chama Cha Wafugaji Tanzania (CCWT) mkoani Dodoma, Regnald Lubeleje (katikati), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), katika mkutano wao uliofanyika mwisho mwa wiki jijini Dodoma. Kushoto ni Mwenyekiti wa CCWT Wilaya ya Bahi, Ibrahim Jama na kulia ni mfugaji, Jacobo Luharatha. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Airbus mbioni kutua Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, amesema kukamilika kwa upanuzi wa mita 250 katika Uwanja wa Ndege wa Dodoma kutaruhusu ndege kubwa zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 200 aina ya Airbus kuruka na kutua kwenye kiwanja hicho.

Aidha, amesema zabuni kwa ajili ya kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Msalato imetangazwa na itafunguliwa mwezi Julai, mwaka huu ili kuendelea na utaratibu wa ujenzi.

Waziri Kamwelwe alitoa kauli hiyo aliitoa juzi, jijini hapa mara baada ya kukagua maendeleo ya upanuzi huo unaotarajiwa kukamilika Agosti mwaka huu na ndege hizo kuanza safari zake Septemba mwaka huu.

Alisema lengo la upanuzi huo ni kuruhusu ndege nyingi zaidi kutoa huduma kwa wakazi wa Mkoa wa Dodoma na mikoa ya jirani.

"Kiwanja hiki kiliongezwa urefu, lakini mahitaji yaliyopo sasa ni makubwa, tumelazimika kuongeza tena urefu ili kukidhi mahitaji kwani idadi ya watu inaongezeka kila siku kwa kuwa Dodoma ni Makao Makuu sasa ya Serikali," alisema.

Waziri huyo alisema pamoja na upanuzi wa uwanja huo, Serikali imetangaza zabuni kwa ajili ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato.

"Pamoja na tatizo la ugonjwa wa corona (COVID-19) kuchangia ucheleweshaji wa ufunguaji na uchambuaji wa zabuni, Serikali inaendelea kuandaa mazingira ili mradi huo uanze," alisema.

Aidha, Waziri Kamwelwe alisema serikali ipo katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za ujenzi wa barabara za mzunguko jijini Dodoma (ringroad) zenye urefu wa kilometa 112 ambao utakuwa na makandarasi watatu.

Kwa upande wake, Meneja wa Wakala wa Barabara (Tanroads) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Leonard Chimagu, alisema kulikuwa na tatizo la maji mengi, lakini wahandisi walipambana na kukabiliana na maji hayo kwa kuanza na uwekaji wa mawe makubwa kabla ya tabaka la kwanza ili kuimarisha barabara ya kuruka na kutua ndege.

"Mradi wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Dodoma, unafanywa na Kampuni ya CHICCO na unatarajiwa kukamilika Agosti mwaka huu na utagharimu kiasi cha Sh. bilioni 3.5," alisema.







Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito (Kushoto), akifuatilia wasilisho la Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Uwezeshaji wa Sekta binafsi ya Kilimo (Pass), Nicomed Bohay (hayupo pichani), wakati wa mkutano wa taasisi hiyo na wadau mbalimbali wanaoshiriki kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika. **PICHA: NEBART MSOKWA**.

# Wizara yapewa somo kusaka masoko ya mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WIZARA ya Kilimo imeshauriwa kuanzisha kitengo maalum cha kutafuta masoko kwa ajili ya mazao ambayo wakulima wanahamasishwa kuzalisha ili kuepuka mazao hayo kukosa soko na wakulima kuingia hasara.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Alibert Chalamila, alipokuwa anafungua mkutano wa asasi ya Uwezeshaji wa Sekta Binafsi ya Kilimo (Pass Trust) na wadau wa kilimo, mifugo na uvuvi.

Pass iliitisha mkutano huo kwa ajili ya kuwaeleza wadau hao wakiwamo wakulima na wadau wengine wanaohusika kwenye mnyororo nwa thamani wa mazao ya kilimo kuhusu fursa ya upatikanaji wa mikopo kwenye sekta ya kilimo.

Chalamila alisema Wizara ya Kilimo imekuwa ikiwahamasisha wakulima kuzalisha mazao mbalimbali kwa wingi, lakini utafutaji wa masoko inaachiwa Wizara ya Viwanda na Biashara, hali ambayo inapunguza ufanisi wa upatikanaji wa masoko.

Alisema ili kuhakikisha wakulima wananufaika na kile wanachozalisha, ni lazima Wizara ya Kilimo ikaanzisha kitengo ambacho kitakuwa kinashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kutafuta masoko ya mazao mbalimbali ya wakulima.

"Sasa hivi tunahimiza zaidi vijana kujiajiri na wengi wao wanajiajiri kwenye kilimo na Wizara inatumia nguvu kubwa kuhamasisha uzalishaji, lakini utafutaji wa masoko inakuwa tatizo, sasa ni vema uhamasishaji ukaenda sambamba na utafutaji wa masoko," alisema Chalamila.

Aliipongeza Pass Trust kwa juhudi zake za kuwasaidia wakulima kupata mikopo kutoka kwenye taasisi mbalimbali za fedha inayowasaidia kuongeza uzalishaji na kwamba hali hiyo imeongeza usalama wa chakula nchini.

Awali akitoa taarifa ya utoaji wa mikopo, Mkurugenzi Mtendaji wa Pass Trust, Nicomed Bohay, alisema taasisi hiyo ilisajiliwa rasmi mwaka 2007 na kwamba mpaka sasa imewasaidia Watanzania 1,200,000 kupata mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 916. Alisema taasisi hiyo inafanya kazi ya kuwaunganisha wakulima na taasisi za fedha pamoja na kuwadhamini kupata mikopo ya kuendeleza kilimo ili kuinua uchumi wao na wa taifa.

"Serikali iliamua kuiendeleza taasisi hii kutokana na kwamba inatambua kuwa Sekta binafsi ndio injini ya uchumi, tunachokifanya ni kuwasaidia wakulima na wadau wengine wanaoshiriki kwenye mnyororo wa thamani kwenye mazao ya kilimo kupata mikopo," alisema Bohay.

Alisema kwenye mkutano huo walishiriki wadau mbalimbali wakiwamo wakulima, waagizaji wa mbolea, wauzaji wa pembejeo, wanunuzi wa mazao ya wakulima, wasindikaji wa mazao, wauzaji wa zana za kilimo na wawakilishi wa benki zote zinazoshirikiana na Pass Trust.

Kwa upande wake, Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alisema mikopo ambayo wakulima wanaipata inasaidia kukuza uzalishaji wa mazao yao na kuinua kipato chao.

Aliwataka wadau wote wanaosaidiwa kupata mikopo hiyo kuwa waaminifu kwenye urejeshaji wa mikopo hiyo pamoja na kuhakikisha wanaitumia mikopo hiyo kwa malengo wanayokusudia.

# Mbalizi wataka Bonde Utengule kulindwa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAKAZI wa Bonde la Utengule katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, wameiomba Serikali kuweka utaratibu wa kuyalinda maeneo ya kilimo ili kuepuka maeneo hayo kuvamiwa na makazi ya watu na kusababisha wananchi kukosa chakula.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, walisema baadhi ya maeneo ya bonde hilo ambalo ni maarufu kwa kilimo cha umwagiliaji yameanza kubadilishwa matumizi na kuyafanya kuwa makazi ya watu.

Joseph Shani, alisema endapo maeneo hayo hayatadhibitiwa vizuri kuna hatari yakatoweka na kubaki makazi ya watu na hivyo kusababisha upungufu wa chakula.

Alisema sehemu kubwa ya eneo hilo miaka ya nyuma ilikuwa inatumika kwa ajili ya kilimo lakini sasa hivi kuna makazi mengi na baadhi ya watu wanaendelea kujenga.

"Tuliona kwenye vyombo vya habari kule Iringa Mkuu wa Wilaya alizuia wananchi kujenga kwenye moja ya maeneo ambayo ni maarufu kwa kilimo, sasa tunatamani na sisi hilo lifanyike ili kuliokoa eneo hili.

Alisema hata katika wilaya ya Kyela iliwahi kutokea miaka ya hivi karibuni ambapo aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Amos Makalla, alizuia wananchi kuendelea kujenga makazi kwenye bonde la Tenende ambalo ni la kilimo na katazo hilo linaheshimiwa.

Naye Zuberi Mwashitete, alisema baadhi ya wananchi wanavamia maeneo hayo kutokana na kukosekana kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi hivyo akaiomba Serikali kuwapelekea mpango huo.

Alisema endapo mpango huo utakamilika kuna uwezekano baadhi ya makazi yakaondolewa na bonde hilo likabaki kuwa ni kwa ajili ya kilimo na makazi yakaendelea kuwa kwenye maeneo yatakayokuwa yameainishwa.

# Wahadhiri wataja wanafunzi wa kike chanzo rushwa ya ngono vyuoni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MHADHIRI mmoja wa chuo kikuu nchini amewatetea wenzake, kwa kueleza jinsi wanafunzi wa kike wanavyochangia kasi ya rushwa ya ngono vyuoni.

Wamesema wanafunzi wa kike ndio kichocheo kutokana na kuvaa mavazi yasiyofaa na kusababisha vishawishi.

Alifichua siri hiyo kutokana na lawama zinazoelekezwa kwa wahadhiri nchini kuwa ndio wanaochochea kasi ya matukio ya rushwa ya ngono vyuoni.

Alizungumza hayo baada ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, kuwatupia lawama wahadhiri wa vyuo nchini kuwa ndio wanaoshawishi rushwa ya ngono kwa wanafunzi wa kike, wakiwaahidi kuwapatia alama nzuri kwenye mitihani.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, alitoa lawama hizo mwishoni mwa wiki wakati wa kampeni maalum ya kupinga rushwa ya ngono vyuoni iliyofanyika katika Chuo cha Uhasibu (TIA) tawi la Mbeya.

Kampeni hiyo iliwahusisha wahadhiri wa vyuo na vyuo vikuu sita vilivyopo jijini Mbeya pamoja na wanafunzi ambapo Matechi alisema kama wahadhiri wangekuwa imara, rushwa hiyo isingekuwa inajitokeza mara kwa mara.

"Rushwa ya ngono kwenye taasisi za elimu ya juu huwa inaonekana zaidi kipindi cha mitihani, kuwapangia wanafunzi mafunzo kwa vitendo pamoja na wakati wa udahili na tatizo huanzia kwa wahadhiri, mpaka sasa tuna kesi mbili za vitendo vya rushwa na moja ilishatolewa hukumu na moja upelelezi unaendelea," alisema Matechi.

Aliwataka wahadhiri na wanafunzi kushirikiana na taasisi hiyo kutokomeza rushwa hiyo kwa maelezo kuwa ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria mtu yeyote kutoa ama kupokea rushwa ya aina yoyote.

Alisema kati ya kesi mbili ambazo wanazo ni ile iliyokuwa inamhusu mmoja wa wahadhiri wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) cha jijini Dar es Salaam, na kwamba kesi nyingine upelelezi umekamilika na wanatarajia kumfikisha mahakamani mhusika.

**UTETEZI WA WAHADHIRI**

Baadhi ya wahadhiri walikanusha kauli kwamba wao ndio wanaowashawishi wanafunzi, na kwamba wanafunzi ndio huwa tatizo kubwa kutokana na mavazi wanayovaa ambayo hayasitiri vizuri miili yao.

Dk. Elimeleck Alkyoo, Mhadhiri wa Chuo cha Uhasibu, alisema wanafunzi wa kike huwa wanatumia mbinu mbalimbali kushawishi wahadhiri kuingia kwenye mitego ya rushwa hiyo.

Alisema wanafunzi hao huwa wanawashawishi kuwapatia alama nzuri kwenye mitihani yao ili wawe na ufaulu mzuri na kwamba wakati mwingine baadhi ya wahadhiri huwa wanashawishika kutokana na kwamba na wao ni binadamu.

Alisema baadhi yao huwa wanavaa mavazi ambayo yanawabana, hivyo kuwasababishia kukosa ustahimilivu na kujikuta wanaingia kwenye mtego wa kushirikiana nao kwenye mapenzi.

"Sisi pia ni binadamu, tumezaliwa kama wengine, tunayokutana nayo vyuoni ni magumu, hivyo tukivuka mihula bila matatizo huwa tunamshukuru Mungu, ushawishi ni mkubwa, watoto wa kike wanavaa mavazi yenye ushawishi mkubwa," alisema Dk. Akyoo.

# Shein avimiminia sifa vyama vilivyounda serikali ya umoja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amevipongeza vyama vya siasa vya upinzani vinavyounda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana navyo, na kuonyesha uzalendo wa hali ya juu.

Akilihutubia Baraza la Wawakilishi na kulivunja mwishoni mwa wiki, Dk. Shein aliwataja viongozi wa vyama hivyo kuwa wameonyesha uwajibikaji mkubwa na kufanya kazi kwa uzalendo, huku wakiweka mbele maslahi ya taifa.

Aliwataja viongozi wa vyama hivyo Juma Ali Khatib kutoka ADA TADEA ambaye ni Waziri asiye na wizara maalumu, Hamad Rashid Mohamed ambaye ni Waziri wa Afya kutoka ADC na Said Soud Waziri asiye na Wizara maalumu kutoka Chama cha Wakulima ambao walikuwa sehemu ya Baraza la Mawaziri lake.

Alisema viongozi hao kutoka vyama vya upinzani ambao waliunda sehemu ya Baraza la Mawaziri wameonesha utiifu mkubwa wakati wote kwa kufanya kazi na kuheshimu maadili ya utumishi wa umma.

"Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati mawaziri wangu kutoka katika vyama vya upinzani, wamefanya kazi kubwa na kuonyesha utiifu na uzalendo wa kupenda nchi," alisema.

Alivitaka vyama vingine vya siasa kuiga mfano wa viongozi hao ambao daima katika kipindi cha miaka mitano alichofanya kazi nao walitoa ushirikiano mkubwa wa kazi hatimaye kufanikisha utekelezaji wa mipango ya Serikali ikiwamo utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.

Baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa marudio wa Machi 2016 na Dk. Shein kuibuka na ushindi, aliunda Serikali kwa kuvishirikisha vyama vitatu baada ya CUF kususia uchaguzi huo kwa madai kwamba uchaguzi wa kwanza wa Oktoba ilibuka na ushindi.

Akizungumza nje ya uwanja wa Baraza la Wawakilishi baada ya hotuba ya Rais Shein kulivunja Baraza la Wawakilishi, Juma Ali Khatib alisema amefarajika na kujivunia kufanya kazi na Dk. Shein na kuweza kuchota busara na utendaji wa kazi.

Alisema alichojifunza katika kipindi cha miaka kumi ni kwamba uongozi ni kuwa na busara na hekima pamoja na kujenga ushirikiano mkubwa na watendaji wenzako na kuwanyenyekea wananchi.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano ameshuhudia mambo yote muhimu yaliyotajwa katika ilani ya kitekelezwa ikiwamo ahadi zake binafsi kama vile kuwalipa wazee waliofikisha umri wa miaka 70 pensheni jamii.




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Ame (wa pili kulia), akimkabidhi kiti Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Mkwajuni, Hasaan Haji, kwa ajili ya wanafunzi wa shule hiyo. Viti hivyo 580 vimetolewa na Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Bil. 21/- kuziwezesha kaya masikini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZAIDI ya Sh. bilioni 21 zinatarajiwa kutumika kwa walengwa wa kaya masikini kwa mwaka mmoja ikiwa ni ongezeko kubwa baada ya miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kufanya vizuri katika awamu mbili katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Ongezeko hilo ni kutoka Sh. bilioni 12 za awamu zilizopita baada ya Zanzibar kushamiri kwenye utekelezaji wa miradi ya Tasaf katika awamu mbili zilizopita.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Dk. Ladislaus Mwamanga, alisema hayo wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji mbali mbali watakaosimamia utendaji wa mpango wa awamu ya pili ya kipindi cha tatu cha mfuko huo kwa kaya masikini Zanzibar.

Aliwataka watendaji hao kufanya kazi ya uhakiki wa majina ya kaya masikini kwa kuzingatia uadilifu mkubwa ili kwenda sambamba na agizo la rais wa Jamhuri ya Muungano, John Magufuli kwa kutunza mahesabu ya fedha.

Alisema uadilifu mkubwa unahitajika ambapo watu watakaoingizwa katika kaya masikini wanatakiwa kuwa na vigezo na sifa kwa mujibu wa malengo ya mfuko huo.

Mkurugenzi wa uratibu wa shughuli za Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Khalid Bakari Amrani, alisema zoezi la kuhakiki kaya masikini Serikali imeamuwa kuwachukua watendaji wa Serikali kwa ajili ya kupata uzoefu wa kazi za uhakiki.

Aliwataka watendaji watakaofanya uhakiki huo kutumia lugha nzuri kwani wanatakiwa kufahamu kwamba wapo watu wenye uhafamu unaotofautiana.

"Watendaji mtakaofanya uhakiki katika kaya masikini tunaowamba kutumia lugha nyepesi yenye kufahamika kwa walengwa kwa sababu wapo watu wanatofautiana katika ufahamu wa mambo,' 'alisema.

Jumla ya kaya 32,660 zinatarajiwa kuhakikiwa katika zoezi la kufanya uhakiki katika mpango wa TASAF awamu ya tatu nchini kote.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatarajiwa kutumia Sh. trilioni 2.03 kwa ajili ya mpango wa kaya masikini chini ya TASAF kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar katika kipindi cha miaka minne.

# CCM Unguja yatamba kushinda majimbo yote

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Ame, amesema wanaingia katika uchaguzi mkuu ujao huku wakiwa na matumaini makubwa ya kushinda majimbo yote tisa katika Mkoa huo.

Alisema wana matumaini hayo kutokana na viongozi wa majimbo kutekeleza ilani ya uchaguzi vizuri katika maeneo yote muhimu.

Alisema hayo wakati akikabidhi madawati pamoja na viti kwa shule nne za jimbo la Mkwajuni, mkoa wa Kaskazini ambavyo ni sehmu ya mchango wa mwakilishi wa jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya.

Alisema mkoa huo una matumaini makubwa ya kuyachukua majimbo yote tisa kutokana na utekelezaji mzuri wa ilani ya uchaguzi katika sekta za maji safi na salama, umeme,elimu na ujenzi wa vituo vya afya kazi ambayo imefanywa na Serikali Kuu pamoja na viongozi wa jimbo ambao ni wabunge, wawakilisi na madiwani.

Alimpongeza mwakilishi wa jimbo la Mkwajuni kwa kufanikiwa kutekeleza ilani ya chama katika mambo muhimu ambayo katika kipindi cha miaka ya nyuma ilikuwa kikwazo katika kuyafikia maendeleo.

Alisema kupatikana kwa madawati kwa shule za Moga, Mbuyu maji,Gamba, Mlilile na Mkwajuni kutawafanya wanafunzi wa shule hizo kusoma katika mazingira mazuri baada ya muda mrefu kukaa chini ya sakafu.

''Nakupongeza kwa dhati mwakilishi wa jimbo la Mkwajuni kwa kufanikiwa kukabidhi madawati haya ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi katika sekta ya elimu na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi," alisema.

Mwakilishi wa Mkwajuni, Ussi Yahya Haji, alisema aliposhinda uchaguzi wa mwaka 2016 na kuliongoza jimbo hilo lilikuwa na changamoto nyingi zilizokuwa kikwazo kwa maendeleo ya wananchi ikiwamo ukosefu wa majisafi na salama.

Alisema suala la majisafi na salama amefanikiwa kulipatia ufumbuzi huku vijiji vya Moga,Gamba pamoja na Chutama hadi Mbuyu Maji na Mlilile wananchi wake sasa wanafaidika na huduma hiyo muhimu kwa maisha ya watu.

Mwenyekiti wa kamati ya shule Hassan Haji, alimpongeza Mwakilishi huyo kwa kutimiza ahadi zake ikiwamo ya upatikanaji wa Madawati kwa wanafunzi wa shule nne za mkoa huo.

# Walia na kero ya maji Sikonge

**Na Welingtone Masele, SIKONGE**

BAADHI ya wakazi wa Kijiji cha Kapumpa Kata ya Kitunda wilayani Sikonge mkoani Tabora, wanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa majisafi na salama na kulazimika kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.

Wameiomba serikali na wadau wa maendeleo kuwasaidia kuondoa changamoto hiyo ambayo wamedai kupunguza muda wa kufanya shughuli za maendeleo.

Walisema kukosekana kwa huduma ya maji kumekuwa kukiwasababishia adha kubwa ambapo baadhi ya wanawake wanaoishi katika kijiji hicho wakieleza kunyanyaswa na waume zao wanapotumia muda mrefu kufuata maji katika maeneo mengine yaliyopo mbali na kijiji chao.

Aidha walisema wamekuwa wakilazimika kununua maji kwa ndoo moja ya lita 20 kwa Sh.500 hali ambayo walisema imekuwa ngumu kwao kuimudu.

Meneja wa wakala wa usambazaji maji vijijini (RUWASA) wilaya ya Sikonge, Mhandisi Paskali Ngunda, amesema serikali inatekeleza mradi wa kutoa maji katika Bwawa la Igumila kupeleka katika kata za Kitunda na Kiloli, mradi unaogharimu zaidi ya Sh. bilioni sita na unatarajia kukamilika kwa awamu ya kwanza mwaka 2021.

# Mkosamali aikimbia NCCR, aenda CHADEMA

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa zamani wa Muhambwe, Flex Mkosamali, ametangaza kukihama chama cha NCCR-Mageuzi na kwenda CHADEMA ambako ametangaza nia ya kugombea ubunge kwenye jimbo hilo.

Mkosamali alikuwa mbunge wa jimbo hilo mwaka 2010 hadi 2015, alitangaza uamuzi huo wiki iliyopita na kukabidhiwa kadi ya uanachama na Katibu wa CHADEMA, Isimaili Kangeta.

Katika ukurasa wa twiter wa Mkurugenzi wa Mambo ya Nje, Mawasiliano na Itifaki, John Mrema, alimkaribisha Mkosamali kwa kuandika;

"Karibu CHADEMA ndugu Felix Mkosamali...umeuona ukweli na kuamua kuhamia CHADEMA."

Naye, John Pambalu aliandika 'karibu sana kamanda Felix Mkosamali. Umekuwa mpambanaji mahiri katika kipindi chote cha maisha yako ya kisiasa. Sisi tunakukaribisha kwa moyo wa upendo na furaha, karibu tufanye kazi ya kuleta haki na usawa."

# Meya mstaafu Songea ajivunia maendeleo lukuki utawala wake

**Na Gidion Mwakanosya, SONGEA**

MSTAHIKI Meya Mstaafu wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Alhaj Abdul Mshaweji, amesema anaona fahari kupatikana kwa maendeleo katika Kata ya Subira, ndani ya miaka mitano ya uongozi wake.

Amesema katika kipindi cha utawala wake kuanzia mwaka 2015, kata ya subira ilibuni na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni moja, miradi iliyogusa sekta muhimu na kuleta manufaa makubwa kwa wananchi.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum.

Mshaweji ambaye pia alikuwa diwani Subira kupitia CCM, alisema tangu mwaka 2015 hadi sasa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyobuniwa imetekelezwa kwa asilimia 98 kwenye kata ya Subira.

Alisema: "Sh.milioni 750 zilitumika kuchimba visima vya maji katika maeneo ya kata ya subira huku Ujenzi wa barabara zenye urefu wa Km 50.3 ukigharimu zaidi ya Sh. milioni 400, ikiwamo barabara ya kutoka Lizaborini kwenda kata ya subira."


"Katika elimu ya msingi na sekondari kuna majengo mbalimbali yaliyojengwa zikiwamo nyumba za walimu, madarasa, vyoo pamoja na maabara yenye thamani ya Sh. milioni 60. Alisema katika sekta ya afya walitumia zaidi ya Sh.milioni 60 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati katika kata hiyo.

Aidha, aliwashukuru wananchi na viongozi mbalimbali wa kata hiyo na manispaa ya Songea kwa ushirikiano wao katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya wananchi wa kata ya Subira na Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

"Wakati huu wa kuelekea uchaguzi mkuu mpya kutajitokeza wapigaramli wengi wakibeza kazi nzuri iliyofanyika katika kipindi cha miaka mitano iliyopita chini ya uongozi wa Rais John Magufuli. Nawashuri wapuuzeni na muwalaani kwa nguvu zote watu hao," alisema Alhaji Mshaweji.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Subira, Gration Sanga, alipohojiwa na Nipashe kwa njia ya simu kuhusiana na ujenzi wa mradi wa vyoo katika shule yake, alisema kuwa ujenzi umekamilika na kwamba wanafunzi na walimu watanufaika na ujenzi huo mara shule zitakapofunguliwa

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Nangwahi uliopo kwenye kata hiyo, Omary Mhagama, alisema kwa kipindi cha miaka mitano wamepata maendeleo mengi.



Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Humphrey Polepole, akipokea simu ya Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais John Magufuli juzi, wakati akizungumza na wanafunzi wa vyuo vikuu mkoani Iringa. Habari Uk. 3. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Afa kwa kuangukiwa gogo la mti shambani

**Na,Said Hamdani, LINDI**

MKULIMA wa Kijiji cha Ruyaya, Kata ya Liimalyao, Tarafa ya Pande, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, Emmanuel Mwicemba Mununi (38), amefariki dunia papo hapo, baada ya kuangukiwa na mti aliokuwa anaukata shambani kwake.

Taarifa zilizothibitishwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, zinaeleza Mununi alifariki dunia Juni 18 mwaka huu saa 3 asubuhi.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo, Mussa Ngwamba, Joseph Kulowa na Daud Mpingo, wameliambia gazeti hili kuwa siku hiyo,Mununi akiwa anakata mti huo aina ya mfuru shambani kwake ulidondoka na kumfikia kifuani na kufa papo hapo.

Walisema kufuatia tukio hilo kabla ya kumtoa walitoa taarifa kwa uongozi wa Serikali ya Kijiji na Kata, ambao nao walifika kushuhudia na wao kuwataarifu viongozi ngazi ya Wilaya ya Kilwa na likiwemo Jeshi la Polisi na mganga wa Zahanati ya Lihimalyao, jina la Mwarami.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ruyaya, Abdalla Selemani Shamte, alithibitisha kutokea kwa kifo cha mwananchi huyo.

Shamte alisema siku na muda huo Mununi akiwa anakata mti huo ulipofikia hatua ya kuanguka ulikatika kisha kudondoka na kumfikia kifuani na kufariki papo hapo.

Kamanda wa Polisi Mkoani Lindi, SP Stanley Kulyamo, alithibitisha kutokea kwa tukio na kueleza baada ya kumkandamiza ulimvunja mbavu zipatazo nne za upande wa mkono wa kushoto karibu na moyo.

Alisema kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa na mganga wa Zahanati ya Kijiji cha Liimaliyao, chanzo cha kifo chake ni pamoja na kuvuja damu nyingi.

HABARI KIMATAIFA

# Watu saba wauawa kwa mashabulizi ya mabomu

**MOGADISHU, Somalia**

TAKRIBANI watu saba wameuawa katika mashambulio mawili tofauti ya mabomu kusini na katikati mwa Somalia.

Taarifa zinaeleza kuwa wanamgambo walijilipua ndani ya gari katika kituo cha ukaguzi cha kijeshi katika jimbo la Galmudug na kusababisha vifo vya wanajeshi watatu.

Katika tukio lingine, mabomu mawili yalilipuka nje ya makazi ya ofisa wa kijeshi mjini Wanlaweyn, na kuua watu wanne.

Hadi kufikia jana jioni, hakuna yeyote aliyekiri kuhusika na mashambulio hayo, lakini kundi la wanamgambo wa al-Shabab limekuwa likiwalenga wanajeshi.

Ofisa wa Jeshi, Meja Abdullahi Ahmed, alisema kuwa katika shambulio la kujitoa muhanga, wanamgambo walilipua bomu gari waliokuwamo baada ya wanajeshi kukataa kutii amri ya kusimama kwenye kituo cha ukaguzi katika jimbo la Galmudug.

Katika tukio lingine katika mji wa Wanlaweyn, Kaskazini-Magharibi mwa mji mkuu Mogadishu, mabomu mawili yalitegwa mbele ya nyumba ya afisa wa kijeshi.

''Kwanza tulisikia mlipuko kwenye nyumba. Ofisa wa kijeshi hakuwapo nyumbani wakati huo. Walinzi na wakazi wengine walifika kubaini chanzo cha mlipuko ndipo mlipuko wa pili ulipotokea,'' alisema Mohamed Nur.

Somalia haijawa na serikali thabiti kwa zaidi ya miaka 20, wakati ambapo sehemu kubwa ya nchi ilikuwa uwanja wa vita.

Al- Shabab wanafanya mashambulizi ili kuiangusha serikali na kuiweka nchi hiyo katika mfumo wa utawala wa sheria za kiislamu au sheria.

BBC

# Watu kiduchu wajitokeza Rais Trump akihutubia

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amefanya mkutano wake wa kwanza wa kampeni tangu nchi hiyo ilipoweka amri ya kutotoka nje kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, huku akiwa mbele ya watu wachache badala ya umati mkubwa wa watu uliotarajiwa.

Rais Trump alikua amejigamba mapema wiki hii kwamba karibu watu milioni walikua wameomba tiketi za kuhudhuria mkutano huo katika eneo la benki ya Tulsa katika kituo cha Oklahoma.

Lakini viti 19,000 vya uwanja huo viliachwa wazi bila watu na mipango yake ya kuhutubia watu ambao alitarajia wangelazimika kukaa nje iwapo uwanja ungefurika ilibidi iachwe.

Kumekua na hofu juu ya kuendesha mikutano ya kisiasa wakati wa janga la corona.

Wale waliohudhuria mkutano wa kampeni walilazimika kusaini makubaliano ya kuilinda timu ya kampeni ya Rais Trump kwamba haitawajibika na ugonjwa wowote iwapo watapata maambukizi.

Saa kadhaa kabla ya tukio hilo kuanza, maofisa walisema kuwa wahudumu sita wa kampeni ya Trump walipatikana na maambukizi ya virusi vya corona.

Hatahivyo, haijawekwa wazi ni kwanini watu wachache waliojitokeza kuliko ilivyotarajiwa.

Rais Trump aliwaelezea wale waliokuwa uwanjani kumsikiliza kama wapiganaji, huku akiwalaumu waandamanaji na vyombo vya habari kwa kuwafukuza wafuasi wake.

BBC



Rais wa Marekani, Donald Trump, akionesha sheria mpya aliyosaini inayowahusu polisi kutenda kazi vizuri. **PICHA: ALLIANCE**

# Misri yaishtaki Ethiopia Baraza la Usalama

**CAIRO, Misri**

MISRI imesema imeliomba Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuingilia kati mzozo wake wa muda mrefu na Ethiopia kuhusu bwawa la umeme katika mto Nile.

Misri inahofu kwamba bwawa hilo litapunguza kiasi cha maji inachohitaji kwa ajili ya shughuli muhimu katika nchi hiyo.

Hatua ya Misri inakuja siku chache baada ya duru ya mazungumzo kati ya Misri, Ethiopia na Sudan kuhusiana na bwawa hilo kumalizika bila ya kupatikana muafaka.

Addis Ababa inatarajia kuanza kulijaza bwawa hilo la Grand Ethiopian Renaissance Dam (GERD) mwezi ujao.

Wizara ya mambo ya kigeni ya Ethiopia imesema katika taarifa siku ya Jumamosi kuwa ombi la Misri linalitaka Baraza la Usalama kuingilia kati ili kuhakikisha mazungumzo kwa nia njema baina ya nchi hizo tatu za mto Nile.

Misri ilichukua hatua hiyo kutokana na kushindwa kwa mazungumzo ya hivi karibuni kuhusiana na bwawa hilo kutokana na msimamo hasi wa Ethiopia.

Misri inailaumu Ethiopia kwa mkwamo huo , ikisema inakosa nia njema ya kisiasa kufikia makubaliano ya mwisho katika mzozo huo.

Ethiopia ilianza ujenzi wa bwawa hilo litakalozalisha umeme lenye thamani ya dola bilioni 4.8 mwaka 2010, kama sehemu ya mpango wa kupanua uuzaji wake wa nishati nje ya nchi.

Misri inategemea kwa kiasi kikubwa maji ya mto Nile kwa kilimo, viwanda na matumizi ya nyumbani ya maji na inahofia kuwa bwawa hilo litaathiri upatikanaji wa maji katika nchi hiyo. Ethiopia inasema hofu ya Misri haina msingi.

*DW*

# Hispania yaondoa 'Lockdown' wananchi waendelea na maisha

NCHI ya Hispania imeondoa vizuizi vilivyoweka nchini humo, ili kukabiliana kusambaa kwa virusi vya corona na kuwaruhusu watu kusafiri tena kwa uhuru kwenye maeneo yote ya nchi hiyo.

Marufuku hiyo imeondolewa baada ya kutekelezwa kwa muda wa wiki 14, ambapo wananchi walitakiwa kusalia nyumbani.

Hata hivyo, Hispania moja ya nchi zilizoathirika vibaya na virusi vya corona, imesema masharti mengine kama vile kuvaa barakoa kwenye maduka, viwanja vya ndege na kwenye usafiri wa umma na kwenye maeneo mengine ya wazi yataendelea.

Idadi ya watu waliokufa kutokana na virusi vya corona nchini humo ni zaidi ya 28,000 na zaidi ya watu 245,000 wameambukizwa virusi hivyo.

Shule nchini humo zitafunguliwa tena Septemba, mwaka huu. Watalii kutoka nchi za eneo la Schengen lisilo na mipaka wanaruhusiwa kuingia tena nchini humo, huku wasafiri kutoka sehemu mbalimbali wataanza kuingia kuanzia Julai Mosi.

Wakati huo huo, Rais wa Marekani, Donald Trump, amewataka maofisa wa afya kupunguza kasi ya kuwapima watu virusi vya corona.

Akizungumza katika wa kuzinduliwa kwa kampeni yake kuwania kuchaguliwa tena kwenye uchaguzi wa Novemba, Rais Trump alisema maofisa wa afya waachane na mpango huo kwani unasababisha kuongezeka kwa idadi kubwa ya visa vya maambukizi.

"Unapowapima watu kwa wingi, utabaini watu wengi zaidi wameambukizwa. Hivyo nawaambia watu wangu, tafadhali punguzeni kasi ya upimaji wa ugonjwa wa corona. nyie mnapima nakupima tu," alisema Trump.

Aidha, Rais Trump alisema kuwa Marekani imewapima watu milioni 25 virusi vya corona.

Nako nchini Iran, shirika la habari la Iran, Isna limeripoti kuwa Waziri wa Afya, Saeed Namaki, amesema mlipuko wa virusi vya corona utaendelea hadi mwaka 2022.

Alisema kulingana na makadirio rasmi, wananchi wa Iran itabidi waishi na virusi vya corona kwa miaka mingine miwili.

Iran inakabiliwa na mlipuko mbaya wa corona katika eneo la Mashariki ya Kati, huku kukiwa na uvumi kuhusu takwimu rasmi za waathirika pamoja na maofisa wa ngazi ya juu wa serikali ambao wanaugua na kufariki kutokana na virusi hivyo.

*DW*



# Kocha Bayern akataa kumzungumzia Sane

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA Mkuu wa Bayern Munich, Hansi Flick, hana cha kusema kuhusu majaliwa ya Leroy Sane baada ya kuthibitika kwamba winga huyo anataka kuondoka Manchester City.

Pep Guardiola alisema wiki hii kwamba ni wazi mchezaji huyo hataongeza mkataba wake na anandoka klabuni hapo.

Bayern kwa muda mrefu imekuwa ikihusishwa na kutaka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, ingawa mlipuko wa virusi vya corona unaweza kufanya usajili huo usifanikiwe.

Akizungumza baada ya ushindi wa mabao 3-1 kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, dhidi ya Freiburg, Flick hakuonyesha nia ya kutaka kujadili kuhusu mchezaji yoyote ambaye atatua hapo kwenye dimba la Allianz Arena.

"Sitaki kuzungumza chochote kuhusu suala hilo," alisema. "Nipo hapa kwa ajili ya kuzungumzia kiwango chetu kwenye mchezo wa leo.

"Sitaki kuzungumza kuhusu majaliwa ya wachezaji wengine au wachezaji ambao wanaweza kuja kujiunga na sisi hapa.

"Bado tuna vitu vya kuvikamilisha msimu huu. Tumeshinda ligi, sasa kinachofuata ni fainali ya DFB-Pokal.

"Baada ya hilo, kutakuwa na kitu kimoja kikubwa, ni kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo tutatakiwa kupigana kwa bidii kuhakikisha tunalitwaa taji."

***

# ARTETA AILAUMU ARSENAL KWA KIPIGO

**LONDON, England**

MIKEL Arteta ameibwatukia Arsenal kuwa "haikubaliki" baada ya kuchapwa 2-1 na Brighton and Hove Albion kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumamosi.

Washika Bunduki hao walikuwa mbele pale kwenye Uwanja wa Amex kwa bao la Nicolas Pepe, lakini wakajikuta wakipoteza kwa mabao ya Lewis Dunk na Neal Maupay.

Hicho kilikuwa ni kipigo cha pili mfululizo kwa Arsenal baada ya kutoka kufungwa na 3-0 na Manchester City Jumatano na Arteta hakuwa na furaha na matokeo hayo.

"Nimepagawa sana," alisema akiiambia BBC Sport. "Haikubaliki kwa namna tulivyopoteza mchezo.

"Tunapenda kushindana na najua kwamba tuna kikosi kichanga, tumepoteza mchezo. Tulitakiwa kushinda mchezo ule mapema.

"Kiukweli kuna jambo lazima lifanyike, kwa sababu inaonyesha wazi kuwa timu haipo kwenye ubora wake, ndani ya siku nne tumefungwa mara mbili. Hapana hili haliwezi kukubalika.

"Haiwezekani tukawa na wachezaji wazuri lakini hatupati matokeo uwanjani, hilo sio jambo zuri kwa timu kwa hakika kabisa hili halikubaliki."



# RAMOS
## ATAKIWA KUSTAAFIA MADRID

**MADRID, Hispania**

SERGIO Ramos anatakiwa kupewa mkataba mpya na Real Madrid ili aweze kumalizia soka lake klabuni hapo, kwa mujibu wa Predrag Mijatovic.

Mkataba wa sasa wa mlinzi huyo wa kati wa Madrid, unamalizika msimu wa 2020-21, ambapo atakuwa na umri wa miaka 35.

Madrid katika siku za hivi karibuni iliwaachia magwiji wake kuondoka klabuni hapo kama Raul na Iker Casillas, ambao walimalizia soka kule Schalke na Porto.

Hivyo, Mijatovic anaona kwamba Madrid wanatakiwa kumwongezea mkataba Ramos ili asiende kumalizika soka lake sehemu nyingine zaidi ya kwa Los Blancos hao.

"Haiwezekani kuwaachia wachezaji walioisaidia timu kirahisi hivyo, kwa sababu ni watu wetu," amesema fowadi huyo wa zamani wa Madrid akiambia Stats Perform News.

"Bahati mbaya hilo huwa halitokei kwa Real Madrid. Raul alikuwa na historia kubwa na pale Real Madrid na aliondoka kwa njia mbaya, Fernando Hierro hivyo hivyo kama ilivyokuwa kwa Casillas.

"Sasa wanazungumzia kuhusu Sergio Ramos (anaweza kuondoka kwa staili hiyo). mkataba wake unatakiwa kuongezwa, kwa miaka miwili au mitatu. Jamaa anatakiwa kumalizia soka lake pale Real Madrid."



HABARI MICHEZO



## KOCHA SIMEONE AISIFIA ATLETICO KWA USHINDI

**MADRID, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Atletico Madrid, Diego Simeone, ameisifia timu yake kwa ushindi ilioupata dhidi ya Real Valladolid wakati wakiwa na uwezekano wa kumaliza kwenye nne bora ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Vitolo alitoka benchi na kufunga bao pekee kwenye mchezo huo dakika ya 81 na kuwafanya Atletico kuibuka na ushindi wa nyumbani kwa Valladolid, Jumamosi.

Atletico imekaa kwenye nafasi ya tatu katika msimamo, ikiwa pointi sawa na Sevilla baada ya mechi 30 na pointi nne zaidi ya Getafe kwenye mbio za kuwania kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

"Mara zote ni muhimu kupata kitu fulani kwenye mchezo na bora zaidi ukishinda," alisema Simeone.

"Kulikuwa na kitu cha kujiimarisha, lakini tulikuwa na miezi mitatu bila maandalizi, halafu unatakiwa kucheza kila baada ya siku tatu.

"Kunahitajika kuzoea mazingira, hasa kutokana na wakati tulionao. Huu ulikuwa ni ushindi muhimu sana kwetu.

"Tulikuwa na nafasi kipindi cha kwanza na hatukuweza kufunga mabao, halafu kipindi cha pili kilikuwa kigumu zaidi kwetu, lakini tukaweza kupata bao."

# KLOPP:

## NGUMU LIVERPOOL KUFIKIA REKODI YA UNITED

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, anaamini haiwezekani klabu yake kuiga mafanikio ya zama za utawala wa Manchester United wakati wakikaribia kutwaa taji la Ligi Kuu England msimu huu.

Liverpool inaongoza msimamo kwa tofauti ya pointi 22 kileleni mwa msimamo na jana Jumapili walisafiri kwenda Goodison Park kucheza na wapinzani wao wa jiji moja, Everton.

Kwa mara ya mwisho Liverpool walitwaa ubingwa wa Ligi Kuu England mwaka 1990 na hawajafanikiwa kulibeba tena taji hilo na sasa wanakaribia kulitwaa kwa mara ya 19, wakiwa nyuma mara moja dhidi ya rekodi ya United.

Wapinzani wao United walitawala ligi hiyo chini ya gwiji Alex Ferguson, wakishinda mara 13 taji la Ligi Kuu kati ya mwaka 1992 na 2013.

"Sifikirii kama inawezekana kutawala tena, kwani ni jambo gumu kiukweli," alisema Klopp, ambaye aliiwezesha Liverpool kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa msimu uliopita.

"United walikuwa na muunganiko mzuri, wakiwa na kocha wa aina yake pamoja na wachezaji wa kiwango cha juu kabisa kwenye timu."

## Maguire awataka United kuimarika wakiivaa Sheffield



**MANCHESTER, England**

NAHODHA wa Manchester United, Harry Maguire amewaonya wachezaji wenzake kwamba lazima waimarike wakati mashetani wekundu hao wakitarajia kucheza na Sheffield United kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

United ipo nafasi ya tano kwenye msimamo wakiwakaribisha Sheffield United waliopo nafasi ya saba kwenye Uwanja wa Old Trafford Jumatano, huku kikosi hicho cha Ole Gunnar Solskjaer kikiongoza kwa pointi mbili katika mbio za kuwania kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Maguire na United yake wamepitwa pointi mbili na Chelsea, ambao wapo nafasi ya nne kwenye msimamo na hivyo wana nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya wao kutoka sare ya 1-1 na Tottenham Hotspur.

United tayari walishacheza na Sheffield United msimu huu, na walifungana mabao 3-3 pale kwenye dimba la Bramall Lane, Novemba baada ya Oli McBurnie kusawazisha dakika ya 90 na Maguire amewataka wachezaji wenzake kuimarika.

"Ulikuwa ni mchezo wa ajabu," amesema Maguire, ambaye aliichezea klabu yake ya utotoni Sheffield United kati ya mwaka 2011 na 2014, akiiambia televisheni ya United.

"Kwa hakika hatukuwa na wakati mzuri kipindi cha kwanza. Sina shaka na hilo, ilikuwa ni wakati tuliocheza vibaya zadi msimu huu.

"Tunatakiwa kuhakikisha tunashinda mchezo huu ili kujiweka kwenye nafasi nzuri zaidi, kwa sababu sio mchezo rahisi kwetu."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LIVERPOOL, MANE MAMBO MAGUMU

## Ni baada ya mshambuliaji huyo 'kuuchuna' kusaini mkataba mpya huku Madrid na PSG zikijipanga...

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Liverpool imeanza kupata hofu ya kumkosa Sadio Mane katika majira ya joto, baada ya mshambuliaji huyo kuonyesha dalili za kutosaini mkataba mpya wa kuendelea kubakia Anfield.

Ingawa mkataba wa sasa wa Mane unatarajiwa kumalizika mwaka 2023, bado hajaweka saini katika mkataba ambao amepewa, ikiwa miezi tisa imeshapita.

Kwa mujibu wa gazeti la The Sun, Real Madrid na Paris Saint-Germain zinajipanga kutoa dau la pauni milioni 150 kwa ajili ya kumsajili Mane endapo atafanya uamuzi wa kuondoka Merseyside.

Taarifa zinaendelea kueleza kuwa, Jurgen Klopp amekuwa na wasiwasi kutokana na mwenendo huo na anataka kujua nafasi iliyopo kuhusiana na hatima ya Mane kama anataka kubakia klabuni hapo.

Katika mkataba wa mpya ambaye Mane amepewa, atakuwa analipwa mshahara wa pauni 220,000 kwa wiki, kiasi ambacho kitakuwa kinakaribiana na mchezaji mwenzake wa timu hiyo, Virgil van Dijk, ambaye pia yuko katika mazungumzo, lakini akikaribia kukubali ofa mpya aliyopewa.

Kwa umri wa miaka 28 alionao Mane, itakuwa ni kiasi kikubwa cha mshahara kupokea endapo atakubali kusaini mkataba huo na anatarajiwa kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa mshahara mnono.

Moja ya vipaumbele vya Klopp ni kuhakikisha Mane ambaye anacheza sambamba na Mohamed Salah na Roberto Firmino katika safu ya mbele ya timu hiyo anabakia klabuni hapo na kuimarisha 'utatu' wao uliopo.

Kocha huyo alisema nyota hao watatu wameisaidia timu kuchukua taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na kukaribia kutwaa kombe la Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza ndani ya miaka 30.

Lakini Mjerumani huyo anajiandaa kukutana na ushindani kutoka kwa klabu kubwa baada ya Mane kuhusishwa kwenye mchakato wa kuhamia PSG, akitajwa kwenye usajili unaomhusisha Kylian Mbappe.

Mane amekuwa na wakati mzuri msimu huu wakati Liverpool jana ikijiandaa kushuka dimbani kwa mara ya kwanza baada ya ligi iliyosimama kujikinga na corona kurejea kwa kuivaa Everton kwenye Uwanja wa Goodison Park.

Nyota huyo amecheza mechi 38 na kufunga mabao 18 huku akitoa pasi za mwisho 12 msimu huu.

## KWA UFUPI

**JIMENEZ AGOMBEWA ULAYA**

JUVENTUS imeungana na Manchester United pamoja na Real Madrid katika mbio za kuwania saini ya straika wa Wolves na Timu ya Taifa ya Mexico, Raul Jimenez, ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Calcio Mercato, via Mail on Sunday)***

**WALKER ANUKIA CITY**

INTER Milan imesema inataka kumsajili beki wa Manchester City na Timu ya Taifa ya England, Kyle Walker, ambaye ana umri wa miaka 30**. *(Sun on Sunday)***

**CAVANI KUONDOKA PSG**

STRAIKA wa Uruguay, Edinson Cavani (33), na beki wa Ubelgiji, Thomas Meunier (28), hawataongeza mkataba na Paris St-Germain ifikapo Juni 30, mwaka huu na nii inamaanisha watakosa mechi zilizobakia za Ligi ya Mabingwa Ulaya zitakazochezwa kuanzia Agosti. ***(RMC, via Mail on Sunday)***

**BAILEY AWEKWA SOKONI**

CHELSEA, Manchester City na Manchester United zimeonyesha nia ya kumsajili winga wa Bayer Leverkusen, Leon Bailey (22). Klabu hiyo ya Ujerumani imetaja thamani ya nyota huyo wa kimataifa kutoka Jamaica ni pauni milioni 40. ***(Mail on Sunday)***

**BARCA KUIKAMUA UNITED**

MANCHESTER United imeelezwa italazimika kulipa dau litakaloweka rekodi ya dunia la pauni 355 kama wanataka kumsajili winga wa Barcelona na Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 21 ya Hispania, Ansu Fati (17). ***(Sunday Express)***

**HENDERSON KITAELEWEKA**

MANCHESTER United inataka kumpa mkataba mpya golikipa, Dean Henderson (23), lakini tayari Chelsea imeonyesha nia ya kumsajili mlinda mlango huyo ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Sheffield United. ***(Sun on Sunday)***

**HART MAMBO MAGUMU**

GOLIKIPA wa zamani wa Timu ya Taifa ya England, Joe Hart (33), amejulishwa na Burnley kuwa mkataba wake na klabu hiyo hautaongezwa baada ya kufika Juni 30, mwaka huu. ***(Mail on Sunday)***

**JORGINHO KUBAKI CHELSEA**

CHELSEA imesitisha mchakato wa kumwondoa klabuni kwake kiungo wa Italia na Juventus, Jorginho (28), na kumleta kiungo raia wa Bosnia-Herzegovina, Miralem Pjanic (30) ndani ya Stamford Bridge akitokea kwa klabu hiyo ya Serie A. ***(Calcio Mercato, via Sunday Express)***

**CEBALLOS AMKIMBIA ZIDANE**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Hispania, Dani Ceballos (23), ataendelea kubakia kwa mkopo Arsenal akitokea Real Madrid mpaka mwishoni mwa msimu lakini atafanya uamuzi wa kuondoka katika klabu hiyo ya LaLiga kama Zinedine Zidane ataendelea kukiongoza kikosi hicho msimu ujao. ***(Marca)***

**MARI MAMBO MAZURI**

ARSENAL imekubali kulipa pauni milioni 14 ili kumpa mkataba wa kudumu, Pablo Mari ambaye yuko kwa mkopo akitokea Flamengo, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kukumbwa na majeruhi ya kifundo cha mguu kwa muda mrefu. ***(Mail on Sunday)***

**KESSIE ANUKIA EPL**

EVERTON na Newcastle United zimeweka wazi nia ya kuwania saini ya kiungo wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Franck Kessie ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Tuttosport, via Football Italia)***

HABARI MICHEZO

# PAMBA YASHIKA TIKETI YA GWAMBINA LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

BAADA ya juzi kulazimishwa sare ya bao 1-1 na Transit Camp, Gwambina FC ya jijini Mwanza, inahitaji kupata pointi mbili ili kupanda daraja na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Kocha Mkuu wa Gwambina, Novatus Fulgence, alisema jana mechi zote za Ligi Daraja la Kwanza ni ngumu kwa sababu klabu zote zimejipanga kusaka ushindi na kujiweka mahali salama katika msimamo.

Fulgence alisema kikosi chake kilishindwa kupata ushindi katika mechi hiyo ya juzi kutokana wapinzani wao kutumia makosa waliyofanya na hivyo sasa wanajipanga kuingia tofauti katika mechi inayofuata.

Kocha huyo allisema safu yake ya ulinzi haikuwa vema katika siku ya juzi, lakini bado nafasi ya kutimiza ndoto zao na kupanda daraja ipo pale pale.

"Mechi za Ligi Daraja la Kwanza ni ngumu kuliko mechi za mashindano yote hapa nchini, ukipata pointi tatu, ujue lazime kijacho kikutoke, ila bado nafasi tunayo na tunawaahidi mashabiki wetu, tuko eneo salama," Fulgence alisema.

Alisema wanakwenda kuyafanyia kazi makosa waliyoyabaini kwa wachezaji wake na wanaamini mechi inayofuata watakuwa katika kiwango bora.

"Sasa hivi naenda kutafuta pointi mbili katika mechi zetu tatu zilizobakia, tunahitaji kupambana, kila mchezaji ajitoe ili kufikia malengo, hasa katika mchezo watu dhidi ya Pamba," alisema Fulgence.

Aliongeza wanahitaji matokeo mazuri katika mchezo huo ili kufikia alama ambazo hazitafikiwa na timu nyingine yoyote katika kundi lao kabla ya kukutana na Rhino Rangers na Mashujaa FC.

Gwambina inaongoza Kundi B ikiwa na ikiwa na pointi 41 ikifuatiwa na Geita Gold Mines yenye pointi 33 wakati Kundi A, Dodoma FC na Ihefu ya Mbeya zenye pointi 39, kabla ya mechi zao za jana zinachuana kusaka nafasi hiyo ya kupanda daraja.




Mshambuliaji wa Simba, John Bocco (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Mwadui FC, Augustino Samson, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Mwadui yafunguka Simba ilipowazidi

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, amesema safu yake ya ulinzi haikuwa katika kiwango kizuri na kusababisha kupoteza mechi yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Simba iliifunga Mwadui mabao 3-0 na kuendelea kujiimarisha kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Adam alisema timu yake ina tatizo katika eneo la beki wa kati kwa muda mrefu na hali inazidi 'kumuumiza kichwa.'

Adam alisema Simba ilicheza vizuri katika mchezo huo ambao ulikuwa na ushindani na anaahidi wanakwenda kujipanga ili kufanya vema katika michezo mingine.

"Niliwaambia wachezaji wangu wawaangalie Simba katika mipira ya katikati kwa sababu nafahamu uchezaji wao, walishindwa kufuata maelekezo na wenzetu wakaitumia vizuri nafasi hiyo," alisema Adam.

Kocha huyo aliongeza atafanyia kazi upungufu aliyouona ili wapate matokeo mazuri katika mechi zinazokuja na hatimaye malengo ya kubakia kwenye Ligi Kuu Bara msimu ujao yatimie.

"Tunakiri tumepoteza mchezo, matokeo ambayo sio mazuri nina kazi kubwa kuhakikisha kikosi changu kinaendelea kushiriki Ligi Kuu," alisema kocha huyo.

Aliongeza wanakwenda kujipanga kuikaribisha Lipuli FC na kuwataka mashabiki wao wasikatishwe tamaa na matokeo ya mechi iliyopita huku akiweka wazi wanawaheshimu wapinzani wao.

## Simba Queens yaipania Ruvuma

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' amesema kikosi chake kiko vizuri na kila mechi kwao ni sawa na fainali sababu wanahitaji kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini, Dar es Salaam jana, Mgosi alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo utakaochezwa Juni 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majimaji mkoani humo.

Mgosi alisema wamejipanga kuondoka na ushindi katika michezo mitatu ya kwanza ili kutangaza ubingwa wa ligi hiyo mapema msimu huu.

Kiungo huyo wa zamani wa mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba, alisema kikosi chake kinatarajia kuondoka jijini Ijumaa kuelekea Ruvuma kwa ajili ya kukabiliana na wenyeji wao.

"Tumerejea na upepo wa kisulisuli, hatuachi mtu salama, kikosi kipo imara malengo yetu ni kushinda michezo mitatu ikiwamo dhidi ya Ruvuma Queens, Yanga Princess na JKT Queens, nina uhakika wa kutwaa taji hilo," alisema Mgosi.

Alisema wanawaheshimu Ruvuma Ila wamejipanga kuhakikisha wanapata alama muhimu katika michezo hiyo ili kufikia malengo yao ya kutwaa taji la ubingwa msimu huu.

JKT Queens ndio mabingwa watetezi na vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na Simba Queens wakati Alliance Queens iko katika nafasi ya tatu.

## Jamhuri, Mwenge zagomea Unguja

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KLABU za Jamhuri na Mwenge zimeliandikia barua Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kueleza zinaomba mechi zao za nyumbani za Ligi Kuu visiwani humo kuchezea Pemba badala ya Unguja kama ilivyoamriwa.

Katika barua yao, klabu hizo zimesema zinahitaji kuchezea Pemba ili kupunguza gharama ambazo watakazoingia endapo watakaa Unguja.

Timu hizo pia ni miongozi kwa klabu tisa zilizoandika barua kwa ZFF zikitishia kugoma kuendelea na Ligi Kuu Zanzibar hadi utakapofanyika Mkutano Mkuu wa dharura.

Kaimu Katibu wa ZFF, Ali Ame Vuai, alikiri kupokea barua hizo na kusema uamuzi wa ligi hiyo kuchezwa katika kituo kimoja ulitangazwa na Wizara ya Michezo ya Zanzibar na si shirikisho hilo. Vuai alisema maombi ya kutaka mechi zao zipelekwe Pemba yatajadiliwa na Wizara ya Michezo baada ya kubaini kama itawezekana kwa kufuata mwongozo uliotolewa wa kujikinga na virusi vya Corona.

"Tumepokea barua hizo mbili, timu zote zipo tayari kuendelea na ligi, lakini zinaomba mechi ambazo zinawakutanisha timu zilizopo kisiwani Pemba zichezwe Gombani, kwa madai ya kupunguza gharama kwa wachezaji ambao familia zinawahitaji na kukaa siku 40 hapa Unguja itakuwa ngumu," alisema kiongozi huyo.

# Michezo

Jumatatu Juni 22, 2020

Nipashe




## Liverpool, Mane mambo magumu

HABARI UK 22



Kiungo wa Yanga, Patrick Sibomana (kulia), akipambana kumtoka beki wa Azam FC, Nicholas Wadada, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa, jijini Dar es Salaam jana. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# YANGA, AZAM ZAIBEBA SIMBA

●●●Ni katika mbio za kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kutoka suluhu kwenye...

**Na Adam Fungamwango**

YANGA na Azam FC zimeendelea kuisafishia njia ya ubingwa Simba baada ya kutoka sare ya bila kufungana katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam jana.

Kwa matokeo hayo sasa, Simba inahitaji pointi nane tu katika mechi zake nane zilizosalia ili kufikisha pointi 83 ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine kwenye ligi hiyo inayotarajiwa kumalizika Julai 26, mwaka huu.

Mabingwa watetezi, Simba wanaendelea kukaa kileleni katika msimamo wa ligi hiyo wakifuatiwa na Azam huku Yanga ikiendelea kubakia kwenye nafasi ya tatu.

Azam ambayo baada ya suluhu ya jana imefikisha pointi 58 na endapo itashinda mechi zake zilizobakia itafikisha pointi 82 wakati Yanga ambayo sasa ina pointi 56, yenyewe ikishinda michezo iliyosalia itafikisha pointi 80.

Mechi ya jana ilishuhudia timu zote zikikosa magoli mengi ya wazi ambayo kama zingetumia vema, basi kungekuwa na idadi kubwa ya mabao katika mechi hiyo.

Dakika ya tisa, Idd Kipangwile alimegewa pande safi na Richard Djodi, lakini kwa mshangao wa wengi alipiga shuti kubwa lililopaa juu ya lango na dakika tatu baadaye, Kipagwile kwa mara nyingine tena, akiwa amebaki na kipa wa Yanga, Metacha Mnata, alishindwa kufunga baada ya shuti lake kumgonga miguuni kipa huyo na baadaye kuokolewa na mabeki.

Baada ya hapo, Yanga ilicharuka na dakika ya 15 ilifanya mashambulizi mfululizo kwa dakika moja na kukosa magoli matatu ya wazi.

Alikuwa ni mshambuliaji, David Molinga aliyeshindwa kuunganisha krosi kutoka kwa winga wa kulia iliyopigwa na Patrick Sibomana, baada ya hapo kilitokea kizaazaa kwenye lango la Azam na mpira ukawa unakwenda wavuni huku kipa Banjamin Haule akiwa hayupo golini, lakini Mudathir Yahaya aliokoa kabla haujavuka mstari wa goli.

Sekunde chache baadaye mabeki wa Azam walijichanganya kwa kurudisha nyuma mpira kimakosa na kumkuta Molinga, akiwa yeye na kipa Haule, lakini shuti lake liliishia mikononi mwa kipa huyo.

Ilikuwa zamu ya Djodi naye kukosa magoli dakika ya 23, alipobaki yeye na kipa, Metacha lakini mpira ulimbabua kipa huyo na ulipomrudia na kupiga 'tiktak' ukaishia tena mikononi mwa kipa huyo.

Feisal Salum nusura aiandikie Yanga bao alipofumua shuti la umbali mrefu, lakini Haule aliudaka kwa ustadi mkubwa, huku Sibomana naye akipewa zawadi ya pasi kutoka kwa mabeki wa Azam, lakini kipa huyo wa Azam jana alikua imara na kuudaka mpira huo.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, huku mshambuliaji nyota wa Yanga, Bernard Morrison, naye akipata nafasi kipindi cha pili na kuifanya Azam kurudi nyuma na kuanza kuzuia kwa muda mrefu mchezo, ikionekana wakihitaji zaidi sare, tofauti na kipindi cha kwanza.

Ilikuwa ni dakika ya 49, wakati Morrison alipopiga krosi iliyokatika na kutaka kuingia wavuni, lakini Haule aliyeonekana kucheza vema jana aliokoa.

Mchezaji wa Azam aliyetokea benchi, Idd Chilunda aliikosesha timu yake magoli mawili, alipobaki na kipa Metacha, dakika ya 68 na 69, baada ya mashuti yake dhaifu kuishia mikononi mwa kipa wa Yanga wakati Nicholaus Wadada naye aliikosesha Azam bao, alipowapiga chenga mabeki wa Yanga, lakini shuti lake dhaifu lilidakwa.

Ligi hiyo itaendelea tena Jumatano kwa Simba kuwafuata Mbeya City jijini Mbeya wakati Yanga itawakaribisha Namungo FC kutoka Lindi na Azam itakuwa mgeni wa Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

## SVEN KUBARIKI UBINGWA MBEYA

**Na Saada Akida**

IKIWA imebakisha pointi 10 ili kujihakikishia kutetea taji la Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema anahitaji kutangaza ubingwa wa msimu huu wakiwa jijini Mbeya, imeelezwa.

Simba itatua Mbeya ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-0, walioupata dhidi ya Mwadui FC, shukrani kwa mabao yaliyofungwa na Hassan Dilunga, John Bocco na Agustino Simon, ambaye alijifunga katika harakati za kuokoa shambulizi langoni mwake.

Vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara wanatarajia kusafiri kuwafuata Tanzania Prisons na Mbeya City, katika mechi mbili mfululizo zitakazochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine kati ya Juni 24 na 28, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili, Sven aliwapongeza wachezaji wake kwa ushindi waliopata dhidi ya Mwadui FC na kuwaeleza anahitaji kuona wanajituma na kujitolea katika michezo inayofuata ili kutangaza ubingwa mapema.

Sven alisema malengo yake ni kutangaza ubingwa mapema kabla ya kurejea jijini Dar es Salaam kukutana na Azam FC katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA.

"Wachezaji wangu wanatakiwa kujituma zaidi, katika michezo yetu ikiwamo dhidi ya Mbeya City na Tanzania Prisons, kucheza kama ilivyocheza dhidi ya Mwadui, ili kutangaza ubingwa mapema. Ingawa najua haitakuwa rahisi," Sven alisema.

Alisema baada ya hapo watakutana na mechi zenye ushindani kwa sababu kila upande utashuka uwanjani ukiwa na malengo tofauti kwenye Ligi Kuu na mashindano hayo ya Kombe la FA.

"Mwezi ujao tutakapotoka Mbeya, tutakutana na mechi ya ushindani mkubwa, ni robo fainali ya Kombe la FA, ni mechi nzuri, pia ngumu kwa timu zote," alisema Sven.

Aliongeza amefurahishwa kuona wachezaji wake wamefanikiwa kushika mabadiliko ya mfumo wa uchezaji kwa haraka ndani ya siku tatu na kufanya vema na hatimaye kupata ushindi mnono.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042